**NSSF** yatengeneza faida trilioni 1.01/- mwaka 2021/2022

UKURASA 4

**Naibu** Waziri anusa ufisadi ujenzi wa shule, ataka uchunguzi

UKURASA 4




UKURASA 9


# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Julai 16, 2023 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0581373

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US


## RIPOTI HAKI JINAI:

# Utendaji Polisi wamkera Rais

• **Ataka** ijitathmini, aagiza yote yaliyobainika kufanyiwa kazi... *Endelea Ukurasa 2*






Rais Samia Suluhu Hassan akipokea taarifa ya Tume ya Kuangalia Jinsi ya Kuimarisha Taasisi za Haki Jinai nchini kutoka kwa Mwenyekiti wa Tume hiyo, Jaji Mkuu mstaafu Mohamed Chande Othman, Ikulu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

### TCU YAONYA MADALALI UDAHILI VYUO VIKUU

TUME ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) imewatahadharisha waombaji wa shahada ya kwanza kupitia dirisha la udahili lililofunguliwa jana...

UKURASA WA 5

### MBUNGE AWALIPUA POLISI MBELE YA WAZIRI

MBUNGE wa Mvomero, Jonas Van Zeeland, amewalipua askari polisi wa kituo cha Dakawa mbele ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi...

## CCM yasema hakuna kurudi nyuma katika suala la bandari

UKURASA 2

# ...Tume yaibua madudu ya kutisha

UK. 3

**MICHEZO** YANGA KUSHUSHA MASHINE MPYA UK.24 | MAONI, KATUNI UK.6



Baadhi ya waendesha magari, pikipiki na bajaji wakiwa kwenye foleni ya kujaza mafuta ya petroli katika Kituo cha GBP Bariadi, mkoani Simiyu jana, baada ya bidhaa hiyo kuwa adimu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Utendaji polisi wamkera Rais Samia

**Na Romana Mallya**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amepokea Ripoti ya Tume ya Haki Jinai huku akiweka bayana kwamba haridhishwi na utendaji wa Jeshi la Polisi na kuagiza kutazamwa upya na kufanyia mabadiliko makubwa.

Sambamba na hayo, ameagiza mapendekezo yote yaliyotolewa na Tume ya Haki Jinai yafanyiwe kazi huku akitaka walioguswa na ripoti hiyo kubadilika kiutendaji.

Rais Samia aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akipokea taarifa ya Tume ya Kuangalia Jinsi ya Kuboresha Taasisi za Haki Jinai, kutoka kwa Mwenyekiti wa Tume hiyo, Jaji Mkuu Mstaafu Mohamed Chande Othman.

Alisema serikali haiwezi kuendelea na hali iliyopo sasa ya Tanzania inapopimwa kwenye masuala kama rushwa na dawa za kuelevya na kutajwa kuwa ni ya 106.

"Kumetajwa muundo wa taasisi za haki jinai. Mimi nikisema muundo wa taasisi jinai sina shida nao, ofisi ya DPP (Mkurugenzi wa Mashtaka), Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mahakama wameshajiweka vizuri. Shida yangu ipo kwa IGP (Mkuu wa Jeshi la Polisi) na Jeshi la Polisi.

"Ninaomba tukalitazame vizuri Jeshi la Polisi. Kuna mmoja alisema liundwe upya. Sisemi liundwe upya lakini kuna mambo mengi yanapaswa kutazamwa na kurekebishwa. Kama ni mafunzo chuoni, utendaji, ningependa Jeshi la Polisi lisimame vizuri pamoja na stahiki zao, mishahara, vikokotoo vikatizamwe ili jeshi lifanye kazi yake vizuri," aliagiza.

Rais Samia alisema mambo yote yaliyoainishwa na tume yanahitaji rasilimali fedha na kumtaka Katibu Mkuu Kiongozi aendelee na kazi kwa kushirikiana na tume hiyo.

"Nikutake Katibu Mkuu Kiongozi ukae na kamati (tume) yenyewe ijivunje vipande vipande iangalie mapendekezo iliyotoa. Yapi wanayaacha serikali itekeleze na yapi yanataka msukumo wao.

"Na mimi nitatoa maoni yangu yapi yanataka msukumo wa kamati ijiunde vipande vipande kwenda kushughulikia masuala mahusus i kwenye mapendekezo iliyotoa ili tuende kwa haraka."Hii ripoti tukichukua niseme niwakabidhi wakuu wa vyombo, polisi hii yako, magereza hii yako, uhamiaji hii yako, zimamoto yako ni hii, TAKUKURU (Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa), zitakwenda kukaa kwenye kabati. Wakifika watawapa wakuu wa vitengo itasomwa kurasa mbili, watatoa na dude lenyewe kubwa litakaa kwenye kabati, haitatekelezwa," alisema.

"Tunataka hii ripoti maoni yake yatekelezwe kikamilifu, ndiyo maana ninasema kamati hii sasa tukajivunje vipande tuingie kwenye sekta, kwenye majeshi yenyewe sasa tukae nao, kamati gani inakwenda kushughulika na Jeshi la Polisi tu, kamati gani inakwenda kushughulikia TAKUKURU," aliagiza.

Pia alitaka zile ambazo si za Muungano, upande wa Zanzibar nao watoe watu watakaoingia kwenye kamati hizo ili kuangalia ni maeneo gani yanatofautiana kisheria na mianya na namna ya kuiziba.

"Katibu Mkuu Kiongozi uendelee na hii kamati kama ni bajeti njoo tutajua tutatoa wapi. Lazima hii hali irekebishwe hatuwezi kuendelea na hali iliyopo sasa ndani ya nchi yetu.

Rais Samia alisema kuna wadau wanasema Tanzania imeshafanya vizuri kiuchumi, kisiasa na kwamba wanataka kusaidia kwenye demokrasia, utawala bora na haki za binadamu.

"Waje hapa watoe hizo fedha. Hili ni swali moja tena kubwa katika haya tuwashirikishe watoe fedha hapa. Ninaishukuru Tume lakini niseme bado kazi iendelee. Hatutaki huko mbele tuseme kulikuwa na Tume, mlizitaja ya Jaji nani, Tume ya Rais Samia yote hayakutekelezwa, twendeni tukajipange tutekeleze," aliagiza.

Kuhusu mapendekezo hayo, Rais Samia alisema yamejigawa maeneo mawili ya kiutawala na kiufundi ambayo yanahitaji mageuzi makubwa ya kubadili fikra na mengine yakihitaji fedha.

Alisema imebainisha kuna udhaifu katika kuheshimu watuhumiwa kwenye ukamataji, upelelezi na uendeshaji wa mashtaka na mambo mengine magerezani wanavyoingia gerezani kuwapekua. Alisema udhaifu huo hauna budi kufanyiwa kazi ili haki itendeke.

"Jambo la pili lililosemwa ni mfumo wa upelelezi unavyotoa mwanya wa rushwa kwa sababu vyombo vyetu mbalimbali kila kimoja kina mfumo wake. Jambo lingine ni ubobezi kwa vyombo vyote, kidogo kuna udhaifu wa ubobezi. Hili si kwa upande mmoja bali kwa pande zote za Muungano. Kuna haja ya kufanya kazi kwa pamoja kuimarisha taasisi hizi kuzipa ubobezi, weledi ili haki Tanzania iboreke," alisema.

Kuhusu vyombo vya ulinzi na usalama, Rais Samia alisema kazi yao ni huduma lakini vimejielekeza kwenye sura ya kijeshi. Aliagiza suala hilo lifanyiwe kazi kwa mujibu wa sheria ilivyoviunda.

**MATUMIZI MABAYA MADARAKA**

"Matumizi mabaya ya madaraka viongozi tupo hapa upande wa serikali na upande wa siasa tunakwenda mbali zaidi. Hili ninadhani ni elimu na mabadiliko ya fikra lakini pia ninadhani linahitaji litungiwe sheria kwa wale wanaoingia kwenye maeneo yasiyo yao na wenyewe washughulikiwe vipi.

"Hili tunaona ni kweli kuna matumizi mabaya ya madaraka wakati mwingine kesi ipo kwa DPP lakini DPP atapigia tu simu futa hiyo kesi. Kwa sababu ana uwezo wa kufuta kesi bila kutoa sababu na ameshapigiwa simu anafuta hiyo kesi.

"Unakuta ule udhaifu, uovu ambao ile kesi imeshtakiwa unaendelea. Lakini aliyefutiwa kesi naye hujiona kwamba atanigusa nani? Futa kesi, kesi zinafutwa, ziwe zozote za uhalifu, za kodi, za nini zinafutwa uhalifu unaendelea," alisema.

Aliongeza: "Hapa nako kuna udhaifu lazima uangaliwe vizuri. Tume imeibua suala la TEHAMA (teknolojia ya Habari na mawasiliano) na haki jinai. Hili ni muhimu nami nimekuwa ninalisema vyombo vya jinai lazima visomane kuanzia mtu anapokamatwa, mashtaka yanavyoendeshwa, upelelezi. Vyote lazima vionekane na Jaji anayekwenda kuhukumu lazima afanye ufuatiliaji wa yote ndipo haki itapatikana."

**ADHABU YA KIFO**

Rais alisema tume imeibua adhabu ya kifo, kifungo cha maisha na kwamba wataalam wataliangalia hilo na kutoa mapendekezo kutokana na maoni ya Watanzania.

Pia alisema suala la uhaba wa watumishi, nidhamu, ukosefu wa maadili, na tatizo la rushwa kwenye vyombo hivyo kamati italiangalia ikiwamo ukosefu wa ofisi katika baadhi ya mikoa.

## CCM: Hakuna kurudi nyuma suala la Bandari

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

CHAMA cha Mapinduzi (CCM), kimesema hakuna kurudi nyuma katika mchakato wa uendeshaji wa bandari kwa ubia na kuiagiza serikali kuanza haraka hatua ya pili ya kuingia mkataba na kampuni ya DP World bila kujali malalamiko yanayoendelea.

Aidha, kimesema kitaendelea kusimamia utekelezaji wa mchakato wa uwekezaji huo kwa kuwa ni moja ya mambo yaliyoainishwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya chama hicho ya mwaka 2020/2025.

Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo, aliyasema hayo jana jijini hapa alipokuwa anahutubia mamia ya wanacahama wa chama hicho kutoka katika mikoa mitano ya Nyanda za Juu Kusini kwenye mkutano uliokuwa na lengo la kutoa elimu.

Alisema uwekezaji wa bandari hiyo una tija kubwa kwa taifa kutokana na kuwa utaongeza mapato, kukuza biashara na kuongeza ajira kwa wananchi pamoja na kuboresha miundombinu mbalimbali nchini.

CCM, alisema ina baraka kwa asilimia 100 kwenye mkataba huo, hivyo serikali inatakiwa kuendelea na hatua inayofuata huku akisisitiza kwamba chama kitasimamia utekelezaji huo mpaka ufanikiwe.

"Uboreshaji wa bandari zetu umeainishwa kwenye Ibara ya 59 ya Ilani ya Uchaguzi ya chama chetu. Imeainishwa kwamba tutaanza na bandari ya Dar es salaam, bandari za Ziwa Nyasa na baadaye kuendelea na bandari zingine," alisema Chongolo.

Alisema mchakato wa uwekezaji huo ulianza tangu mwaka 2019 baada ya kufanya mazungumzo na mwekezaji wa awali, kampuni ya Tanzania International Container Services (TICSO ambayo ilikuwa inaendesha bandari hiyo tangu mwaka 2002.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Prof. Kitilla Mkumbo alisema serikali itaendelea kutekeleza mkataba huo bila kujali kelele ambazo zinatolewa na watu wanaopinga kwa maelezo kuwa una faida kubwa kwa maendeleo ya taifa.

Alisema kabla ya kuichagua DP World, serikali ilifuata sheria kwa kuishindanisha na kampuni zingine zaidi ya sita ambazo pia zilikuwa zinataka kuwekeza.

Prof. Mkumbo alisema kampuni hiyo ilishinda kutokana na kuwa na uzoefu wa uendeshaji wa bandari na magati katika mataifa mbalimbali duniani ambao serikali ilijiridhisha kwamba unaweza ukalisaidia taifa. Alisema kampuni nyingi za kimataifa zimekuwa zikivutiwa kuwekeza Tanzania kutokana na kuwa taifa lenye amani na utulivu pamoja na kuwa na mazingira rafiki kwa uwekezaji.

"Kukaribisha wawekezaji haitakuwa mara ya kwanza katika nchi hii. Ukienda kwenye viwanja vyetu vya ndege utakutana na kampuni za kimataifa zikifanya shughuli mbalimbali za uendeshaji," alisema.

Alisema kwa sasa serikali inakusanya Sh. trilioni saba kwa mwaka kutokana na mapato ya bandari na kwamba baada ya uwekezaji huo, serikali itakuwa inakusanya zaidi ya Sh. trilioni 26.7.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma na Mashirika ya Umma, Jerry Silaa, alisema kwenye uwekezaji unaotarajiwa kufanyika kwa mujibu wa mkataba huo kila upande umepewa majukumu yake.

HABARI KITAIFA

# Tume Haki Jinai yaibua madudu ya kutisha

**Na Romana Mallya**

TUME ya Haki Jinai iliyoundwa na Rais Samia Suluhu Hassan, imeibua mambo mbalimbali ikiwamo udhaifu kwenye mnyororo wa upatikanaji haki katika taasisi zinazohusika na utoaji haki na utekelezaji wa sheria.

Imebaini kuwa, wakuu wa mikoa na wilaya wanalalamikiwa kutumia vibaya madaraka yao ya kutoa amri za kukamata na kuweka maabusu. Pia baadhi ya viongozi wa juu wa kisiasa wamekuwa wakitoa matamko na amri ya kuamuru vyombo vya dola kukamata na kumweka ndani mwananchi wakati mamlaka hayo hawana.

Kutokana na kuwapo kwa kasoro hizo, Tume hiyo imependekeza viongozi hao wa kisiasa na serikali waelekezwe kuzingatia sheria.

Pia, tume imebaini kuna maombi ya kufutwa adhabu ya kifo kwa sababu ni ya kikatili na isiyozingatia haki za binadamu kwa kuwa kunakuwa na kutotekelezeka kwa miaka 28 na kuwatia hofu wafungwa.

Akisoma Ripoti ya Tume jana Ikulu, Dar es Salaam, Mwenyekiti wake, Jaji Mkuu Mstaafu Mohamed Chande Othman, alisema wamebaini kuna upungufu wa mfumo wa uwajibikaji na matumizi mabaya ya madaraka na utamaduni wa kufichiana siri na kustahiana pasipo ulazima.

Ripoti hiyo ilikabidhiwa kwa Rais Samia Suluhu Hassan ambaye alisema yote yaliyopendekezwa yatafanyiwa kazi.

Jaji Chande pia alisema Tume imebaini nyaraka za mahakama kwenye mijadala ya kesi 253, baadhi ya washtakiwa waliokiri makosa hawajamaliza malipo.

"Utaratibu wa kukiri kosa ulikuwa na awamu tatu, ya kwanza ilikuwa 2019/21 na baada ya marekebisho kufanyika kulikuwa hakuna kanuni, na awamu ya pili ni baada ya kanuni kuwekwa na kabla ya notisi ya ugatusi na awamu ya tatu ni kuanzia Juni mwaka 2022," alisema.

Alisema tume imependekeza elimu itolewe na iundwe tumu maalum kuchunguza utata katika baadhi ya mali zilizotaifishwa katika utaratibu huo wa kukiri kosa na utendaji wa kikosi kazi ili kuishauri serikali.

Alitaja kasoro nyingine ni suala la uhuru wa kufuta mashauri mahakamani alio nao Mkurugenzi wa Mashitaka (DPP) bila kutoa sababu na mahakama kutoingilia uhuru huo na kwamba yako malalamiko ya matumizi mabaya ya fursa hiyo.

Pia, alisema tume imebaini uwapo wa taasisi nyingi za ukamataji zenye mahabusu hali inayosababisha ugumu kwa wananchi kujua waliko watuhumiwa wanapokamatwa. Pia alisema mahabusu zingine hazijulikani zilipo na kwamba bado kuna ukiukwaji wa sheria kwa kutofikishwa mahakamani ndani ya saa 24 baada ya mtuhumiwa kukamatwa huku wengine wakikamatwa kabla ya upelelezi kukamilika.

**KIFUNGO CHA MAISHA**

Kuhusu kifungo cha maisha, alisema kuna malalamiko ya adhabu hiyo kuwa hakitoi nafasi ya mfungwa kujirekebisha.

Pia alisema madai ya stahiki mbalimbali ambapo askari wa chini wamemwomba Rais kuangalia masuala ya kikokotoo ambacho wameiambia Tume kuwa kinawaweka roho juu.

Alisema Tume inapendekeza kwa sababu mashauri yanayosikilizwa Mahakama Kuu hayana kikomo cha upelelezi, sheria ya mwenendo wa mashauri ya jinai yarekebishwe na kuweka kikomo kwa mashauri yanayosubiri kusikilizwa mahakamani.

Tume ilisema imebaini wakuu wa wilaya wamekuwa wakiambatana na wajumbe wa kamati za ulinzi na usalama katika ziara mbalimbali hata zile zisizo stahili na kwamba uwapo wa kamati hizo na kujitambulisha kama Wenyeviti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama kinyume cha Sheria Sura ya 16 inayowatambua kama Wenyeviti wa Kamati za Usalama Mikoa au Wilaya.

"Tume tunapendekeza Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya wazingatie kuwa wanapotekeleza mamlaka ya ukamataji ni muhimu kufuata matakwa ya kifungu cha 7 na 15 ambayo ni kosa liwe limetendeka mbele ya kiongozi, liwe la Jinai na liwe limetendwa na limesababisha uvunjaji wa amani na utulivu," alisema.

Kadhalika alisema tume inapendekeza mahakimu ambao nao ni walinzi wa amani, waondolewe mamlaka hayo kwa sababu hayatumiki mara nyingi na kupendekeza Jeshi la Polisi lifikishe huduma zake katika ngazi ya kata. Mwenyekiti huyo alisema Tume imebaini kutotenganisha idara ya upelelezi ya Jeshi la Polisi na shughuli zingine za jeshi hilo, kumesababisha ucheleweshaji wa upelelezi, ukosefu wa ubobezi, ufanisi mdogo katika upelelezi na wapelelezi wa jeshi la polisi wakati mwingine kupangiwa shughuli zingine ambazo hazihusiani na upelelezi.

"Asilimia 59.7 ya askari polisi na magereza tuliowahoji wameeleza uhusiano katika ya taasisi haki jinai si nzuri. Asilimia 55.3 wamependekeza uhusiano wa kiutendaji uboreshwe baina ya taasisi hizi," alisema.

Alisema tume inapendekeza serikali iunganishe nguvu ya upelelezi na uchunguzi iliyopo sasa kwa vyombo hivyo kwa kuanzisha mamlaka mpya na huru ya upelelezi itakayojulikana na kujitegemea kama Ofisi ya Taifa ya Upelelezi ambayo itakuwa na jukumu la kupeleleza makosa yote makubwa ya jinai yakiwamo rushwa na dawa za kulevya na kujifunza uzoefu kutoka Rwanda, Marekani, Pakistani, India na Ufilipino.

Alisema tume inapendekeza Jeshi la Polisi na vyombo vingine vya ukamataji viwafikishe watuhumiwa mahakamani kwa wakati kwa mujibu wa sheria na watuhumiwa wasikamatwe kabla ya kupelelezi kwa makosa makubwa.

Rais Samia aliunda Tume hii mwezi Januari, mwaka huu ikiwa na wajumbe 11 ikiongozwa na Jaji Mstaafu Chande na Katibu wake, Balozi Omeni Sefue ambaye ni Katibu Mkuu Kiongozi mstaafu.



Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Prof. Dorothy Gwajima, akiagana na Naibu Qadhi Mkuu Sheikh Ali Ngeruko (kulia), baada ya kuzindua kongamano kuhusu kukithiri kwa ndoa kuvunjika, lililofanyika katika Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA), Kinondoni Dar es Salaam jana. Kushoto ni Mwenyekiti wa Vijana BAKWATA Taifa, Prof. Muharami Pembe. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# TCU yaonya madalali udahili vyuo vikuu

**Na Romana Mallya**

TUME ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) imewatahadharisha waombaji wa shahada ya kwanza kupitia dirisha la udahili lililofunguliwa jana, kuwa makini na watu wanaojiita madalali kwa kuwa maombi yote ya taasisi za elimu ya juu hufanyika moja kwa moja kupitia vyuo vikuu husika.

Katibu Mtendaji wa TCU, Prof. Charles Kihampa, alitoa tahadhari hiyo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu kufunguliwa kwa dirisha la udahili kwa waombaji wa shahada ya kwanza.

"Ninaomba kuwatahadharisha waombaji wote kuwa maombi yote ya udahili wa vyuo vya elimu ya juu yanafanyika kupitia mifumo ya kieletroniki. Hakuna watu wa katikati maarufu kama madalali, hivyo waombaji waepuke wasije kutapeliwa.

"Shahada ya juu hatuna mawakala wala madalali, mwombaji anashauriwa kwenda moja kwa moja kwenye tovuti ataona sifa zote huko," alisema.

Kuhusu dirisha hilo, Prof. Kihampa alisema limefunguliwa rasmi kuanzia jana na litaendelea hadi Agosti 4, mwaka huu, na makundi yanayotakiwa kuomba ni pamoja na wenye sifa stahiki za kidato cha sita.

"Wenye sifa stahiki za stashahada au sifa linganifu na wenye sifa stahiki za cheti cha awali cha Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT) wanaruhusiwa kuomba," alisema.

Prof. Kihampa aliwasisitiza waombaji kuhakikisha maombi yanatumwa moja kwa moja kwenye vyuo ambavyo mwombaji amevichagua na kuchagua programu za masomo anazozipenda.

"Vigezo na sifa katika programu mbalimbali za masomo vinapatikana katika tovuti za vyuo husika na katika vitabu vya mwongozo wa maombi ya udahili vinavyopatikana kwenye tovuti ya TCU," alisema.

Alisema waombaji wenye vyeti vilivyotolewa na mabaraza ya mitihani nje ya nchi ni lazima wawasilishe vyeti vyao Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA).

"Kwa vyeti vya elimu ya sekondari au Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzi ya Ufundi Stadi (NACTVET) kwa vyeti vya shahada ili kupata ithibati ya ulinganifu wa sifa zao kabla ya kutuma maombi ya udahili," alisema.

Prof. Kihampa aliwataka waombaji, wazazi na walezi kujitokeza kwenye maonyesho ya 18 ya Vyuo Vikuu yanayotarajia kuanza kesho(Jumatatu) katika Viwanja vya Mnazi Mmoja jijini hapa na kumalizika Julai 22, mwaka huu.

Alisema katika maonyesho hayo taasisi za elimu ya juu zaidi ya 80 zinatarajia kushiriki na kutoa fursa kwa waombaji


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA MOROGORO**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA MAHALI....MOROGORO**
**MAOMBI NA. 33/2023.........MWAKA 2023**
**ZEGGE OMARI DIHAMBWA.........MUOMBAJI**
**TATU HASSAN...........MJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI**


**KWA: TATU HASSAN**

Unafahamishwa kwamba shauri hili limepangwa kutajwa/kusikilizwa tarehe 17 mwezi wa 07 mwaka 2023 saa 08:00 asubuhi mbele ya Mh. M. Khassim Mwenyekiti wa Baraza.

Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.

Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na Lakiri/muhuri wa Baraza hii leo tarehe 03 mwezi wa 07 mwaka 2023.

MWENYEKITI




Ofisa Maendeleo ya Vijana wa Mkoa wa Arusha, Japheth Kurwa (kushoto) na Naibu Meneja wa Mradi wa kusaidia mabinti, walemavu, vijana balehe walioko nje ya shule na wanaoishi na maambuziki ya Virusi Vya Ukimwi (SHDEPHA), Irene Jacob (kulia), wakikabidhi mfano wa hundi ya 500,000/- kwa mmoja wa washindi wa shindano la uwasilishaji wa wazo la biashara lenye ubunifu ‘fire challenge’, Muelimisha rika, Piala Silayo yaliyoandaliwa na Taasisi ya Okoa New Generation (ONG), jijini Arusha jana. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# NSSF yatengeneza faida ya tril. 1.01/-

**Na Mwandishi Wetu**

MFUKO wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) umepata faida ya zaidi ya Sh. trilioni 1.01.

Faida hiyo ni kwa mujibu wa hesabu zilizokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) katika mwaka wa 2021/22.

Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Masha Mshomba, alisema juzi kuwa mbali na faida hiyo, mapato yatokanayo na uwekezaji pia yameongezeka na kufikia Sh. bilioni 745.

“Hii haijawahi kutokea katika historia ya NSSF,” alisema wakati akitoa tathmini yake baada ya kupokea taarifa ya watendaji wa mfuko walioshiriki kuhudumia wanachama na wananchi kwenye Maonyesho ya 47 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam yaliyofikia kilele juzi.

Mshomba alitaja sababu za mafanikio hayo kuwa ni pamoja na juhudi kubwa zinazofanywa na serikali chini ya Rais Samia Suluhu Hassan ambaye baada ya kuingia madarakani, alikuja na mpango wa “kuifungua nchi”. Mpango huo ulilenga kuwaalika wawekezaji kuwekeza nchini lakini pia kutangaza vivutio vya utalii vilivyoko Tanzania kupitia filamu ya The Royal Tour.

“Kichocheo kikubwa ni Mheshimiwa Rais alivyoweza kuwavuta wawekezaji. Kumekuwa na ongezeko kubwa la waajiri na waajiriwa. suala zima la uchangiaji limeongezeka, vipato vya wafanyakazi vimeongezeka na haya yote yamechangia kuongeza michango na kufanya kipato cha mfuko kutokana na uwekezaji kuongezeka pia,” alisema Mshomba.

Alisema sababu nyingine ni juhudi kubwa zilizowekwa na mfuko katika kuboresha mifumo ya teknolojia ya Habari na mawasiliano (TEHAMA) ambayo imesaidia kuboresha utoaji wa huduma.

“Kulingana na mpango wetu wa maendeleo wa miaka mitano ambao unaishia Juni 2026, thamani ya mfuko itafikia zaidi ya Sh. trilioni 11.5. Yote haya yanatokana na msukumo wa kuongeza waajiri na waajiriwa wanaochangia katika mfuko lakini pia kazi nzuri inayofanywa na mfuko,” alisema huku akibainisha kuwa kwa sasa thamani ya NSSF ni Sh. trilioni 7.1.

Mkurugenzi Mkuu aliwahimiza Watanzania hususan kutoka sekta binafsi kujiunga kwa wingi ili kujenga maisha yao ya sasa na ya baadaye. Pia alisema NSSF imepewa jukumu la kushughulika na sekta isiyo rasmi.

“Tunakamilisha taratibu za mwisho na tunaamini tukiweza kuwa na uchangiaji katika sekta isiyo rasmi, basi NSSF itazidi kupaa zaidi na kuwa na mchango mkubwa katika maendeleo ya nchi hii,” alisema.

Idadi kubwa ya Watanzania, alisema iko katika sekta isiyo rasmi na wakifanikiwa kujimuishwa kwenye mpango huo, taifa litakuwa limefanikiwa kuondoa umaskini nchini.

“Kama ninavyosema siku zote hifadhi ya jamii iko kwa ajili ya kuwahudumia wananchama hasa kwa lengo la kuwaondolea umaskini pale wanapokoma kufanya kazi,” alifafanua.

Kuhusu ushiriki wa NSSF katika Maonyesho ya 47 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam, Mshomba alisema zaidi ya wanachama 2,400 wametembelea na kuhudumiwa katika banda hilo.

“Kumekuwa na mabadilio chanya kulinganisha na mwaka jana. Wanachama wetu wamehudumiwa kwa kupatiwa elimu, usajili wa wanachama, umuhimu wa kuwasilisha michango kwa wakati na kuondoa kero mwanachama anapostaafu, elimu katika masuala ya uwekezaji, mafao yatolewayo na mfuko ambayo yanafikia saba lakini pia masuala ya uwekezaji,” alifafanua.

Kuhusu Uwekezaji, Mshomba alisema wamebaini kuwa watu wengi wamevutiwa na eneo hilo na kwamba kuna maeneo ambayo wanachama wanaweza kufaidika moja kwa moja kwa kuwa mfuko unajenga nyumba ambazo zinauzwa na kupangishwa kwa wateja.

## Chanzo wajasiriamali kuingia mikopo umiza chawekwa hadharani

**Na Christina Haule,**
MOROGORO

TABIA ya kujilimbikizia madeni na kuchelewa kulipa mikopo kwa wakati, imebainika kuwa inatokana na wajasiriamali wengi kujiingiza katika kutatua changamoto za maisha ikiwamo kugharimia matibabu jambo ambalo ni kinyume cha masharti ya mikopo hiyo.

Mmoja wa wajasiriamali ambaye ni mkulima wa mazao ya mboga kutoka Dumila wilayani Kilosa mkoani Morogoro, Jonas Laurent, alisema jana wakati akizungumza na Nipashe.

Alisema wajasiriamali na wananchi hutumia mikopo kwa ajili ya kutatua matatizo ya kifamilia na matokeo yake hushindwa kurejesha kutokana na mitaji yao kuwa midogo.

Laurent alisema wako baadhi ya wajasiriamali ambao wamekuwa na tabia ya kukopa zaidi ya taasisi moja ya kifedha sababu mojawapo ikiwa ni kurejesha mkopo wa kwanza lakini baadaye hushindwa. Matokeo ya kutofanya hivyo, hujiingiza katika mikopo migumu maarufu kama ‘kausha damu’ na hatimaye kushindwa kulipa na kujikuta wakiingia katika matatizo.

“Utakuta mjasiriamali kwa wakati huo hahitaji mkopo wa biashara lakini ana mtoto au ndugu yake wa damu anaumwa na inahitajika fedha nyingi kuokoa uhai wake. Kutokana na changamoto hiyo, analazimika kuingia mkopo mwingine ili kuokoa uhai wa mpendwa wake. Sasa shida inakuja kwenye kulipa hadi waanze kuvutana na ndugu wengine, huku riba nayo inaendelea kukua,” alisema Laurent.

Naye Meneja wa taasisi ya kiserikali ya utoaji mikopo ya Self Microfinance Fund (Self MF) Tawi la Morogoro, Moses Ntambi, aliziomba taasisi zingine za kifedha kutumia mfumo wa taarifa za wakopaji wa mikopo uliopo ili kuweka taarifa za wakopaji na kusaidia watoa huduma wengine kutokutoa mkopo mwingine kwa mtu ambaye ameshakopa na kutompa mzigo.

Ntambi alitoa rai kwa mamlaka husika za warasimishaji wa ardhi nchini kujitahidi kuweka sawa taratibu za urasimishaji ili kuwapo na sehemu nyingi zilizorasimishwa na kuepuka kupata nyaraka zisizorasimishwa ambazo hazina namba inayoonekana kwenye taarifa za mkopaji.

Alisema wako wakopaji wanapeleka nyaraka za maeneo yasiyopimwa na kuleta mkanganyiko baada ya kubainika kutumika katika taasisi tofauti na kumfanya mkopaji kuona bora akimbie sababu ya dhamana aliyotoa kutokuwa halisi na kusababisha hasara katika asasi hizo za kifedha.

Ofisa Mikopo wa Self MF, Faraja Kauzeni, alisema taasisi hiyo hugusa makundi yote ya kijamii wakiwamo wafanyabiashara, wakulima, wafugaji na taasisi za kifedha kwa kuwapa mikopo ya miezi mitatu hadi sita kabla ya kurejesha ili mkopaji anufaike kiuchumi.

# Waziri anusa ufisadi ujenzi wa shule, ataka uchunguzi ufanyike

**Na James Mwanamyoto,**
TAMISEMI

NAIBU Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Deogratius Ndejembi, AMEMWAGIZA Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais-TAMISEMI kuunda timu maalum ya kukagua matumizi ya fedha kwenye ujenzi wa shule ya Sekondari ya Wasichana Kwembe inayojengwa katika Manispaa ya Ubungo kupitia mradi wa SEQUIP.

Ndejembi alitoa maagizo hayo, akiwa katika Manispaa ya Ubungo mara baada ya kutoridhishwa na hatua ya ujenzi iliyofikiwa licha ya Rais Samia Suluhu Hassan kutoa fedha nyingi ili kukamilisha ujenzi wa shule hiyo maalum ya wasichana ya sayansi.

alisema hajaridhishwa na hatua ya ujenzi iliyofikiwa ikizingatiwa kuwa awali serikali kuu ilitoa Sh. bilioni tatu na kuongeza Sh. bilioni 1.1 na Manispaa ya Ubungo ikaongeza tena Sh. bilioni 1.2 ili kukamilisha ujenzi wa miundombinu katika shule hiyo.

“Nilichokiona hapa ni dalili za matumizi mabaya ya fedha zilizotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan, hivyo ofisi ya Rais-TAMISEMI haiko tayari kuona fedha ikichezewa ndiyo maana nimeelekeza uchunguzi ufanyike,” alisema.

Ndejembi pia aliutaka uongozi wa Manispaa ya Ubungo kuongeza usimamizi na kumtaka mkandarasi kuongeza idadi ya mafundi ili shule hiyo ikamilike na kuwapokea zaidi ya wanafunzi 200 waliopangiwa kuripoti katika shule hiyo.

Akizungumzia kusuasua kwa ukamilishaji wa ujenzi wa miundombinu ya elimu mkoani Dar es Salaam, Ndejembi alisema wataalam na makandarasi wameikwamisha serikali kutekeleza lengo la kuboresha miundombinu kwa wakati.

Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, Hashim Komba, aliahidi kuwa atahakikisha anawasimamia makandarasi na mafundi kufanya kazi usiku na mchana ili shule hiyo ikamilike na kupokea wanafunzi waliopangiwa kuripoti katika shule hiyo.

Kutokana na hali hiyo, aliwataka wahusika kubadilika kiutendaji ili wawe na tija katika maendeleo ya taifa.

## HABARI KITAIFA



Mbunge wa Jimbo la Mvomero, mkoani Morogoro, Jonas Van Zeeland (kushoto), akitoa maelezo kwa Waziri wa Mambo ya Ndani, Hamadi Masauni (wa pili kulia) na Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Adam Malima (wa tatu kulia), kuhusu Polisi wa kituo cha Dakawa wanaodaiwa kumpiga raia na kusababisha kifo chake, katika mkutano wa hadhara uliofanyika eneo hilo, juzi. **PICHA: ASHTON BALAIGWA**

# Mbunge awalipua polisi mbele ya Waziri

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

MBUNGE wa Mvomero, Jonas Van Zeeland, amewalipua askari polisi wa kituo cha Dakawa mbele ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kuwa wanakiuka misingi ya haki na maadili katika kukamata watuhumiwa wa makosa mbalimbali.

Amesema utendaji wa askari wa kituo hicho kinachotumika kama ofisi ya Mkuu wa Polisi wa wilaya ya Mvomero ni wa kutia shaka, hivyo kuomba hatua zichukuliwe.

Zeeland alitolea mfano wa kifo cha kutatanisha cha Yassin Mangube (34) ambaye anadaiwa kufariki dunia kutokana na kipigo kutoka kwa askari wa kituo hicho baada ya kukamatwa kwa madai ya kuchukua simu ya mama yake mdogo.

"Mheshimiwa Waziri hapa Dakawa ipo changamoto kubwa sana. Yule kijana alipoteza maisha naomba kupitia vyombo vyako ikikupendaza unda tume ichunguze, ukweli ubainike juu ya huyu kijana aliyepoteza maisha kwa kudaiwa kupigwa na askari polisi wa kituo hicho" alisema.

Baada ya maelezo ya mbunge huyo, Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Adam Malima, ambaye aliambatana na Waziri Masauni, alitoa nafasi kwa mlezi wa Yassin, Tabu John, ambaye alisema alimlea kijana huyo kabla ya kukamatwa na kwamba alipita nyumbani kwake na alimtuma kwenda kununua unga.

Alisema chanzo cha tukio hilo, Yassin alikuwa akimdai mama yake mdogo simu na kuamua kuchukua simu anayomiliki mama huyo kwa lengo la kumshinikiza arudishe simu yake lakini muda mfupi askari wa kituo cha Dakawa walifika eneo hilo na kumkamata na kumfikisha kituoni.

"Ndani ya saa moja au mbili, Yassin amerudi nyumbani akiwa anatema damu, ananiamsha na kunambia amepigwa na kuwataja polisi waliompiga. Ilipofika asubuhi hali yake ilibadilika na kupelekwa hospitali. Mimi nilienda kwenye kikao baadaye napigiwa simu kwamba Yassin amefariki dunia wakati saa 3:00 nilikuwa naye na askari hao bado wapo tu mpaka leo," alisema Tabu.

Akijibu tuhuma hizo, Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Kamishna Msaidizi (ACP) Hassan Omary, alikiri kutokea kwa tukio hilo huku akidai kuwa mtuhumiwa alikwenda kumfanyia fujo mama yake mdogo na baadaye alikamatwa na askari kisha kufikishwa kituoni. Alisema baada ya muda mfupi hali yake ilibadilika na kufikishwa katika zahanati kwa ajili ya matibabu lakini umauti ulimfika.

Alisema baada ya kufariki dunia, jalada lilifunguliwa dhidi ya askari na walishikiliwa kama watuhumiwa wengine na uchunguzi wa mwili ulifanyika katika Hospitala ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro na mtalaam kutoka Muhimbili mbele ya ndugu wa marehemu.

Kamanda Omary alisema matokeo ya uchunguzi yalionyesha kifo chake hakitokani na kipigo na jarada la kesi lilipelekwa ofisi ya Mwanasheria wa Serikali ambaye ndiye mwenye mamlaka na kesi.

"Baada ya jarada kufikishwa kwa Mwanasheria wa Serikali waliona hakuna ushahidi wa kuwafikisha mahakamani.

Hapa ninachokiona ni changamoto ya mawasiliano kati ya Polisi mkoa na Ofisi ya Waziri wa Mambo ya Ndani," alisema.

Baada ya kusikiliza maelezo ya pande zote mbili, Waziri Masauni alisema bado tukio hilo lina ukakasi na kuwataka wananchi wenye ushahidi wajitokeze kwenye vyombo shirikishi kwa kuwa kesi ya jinai haina mwisho na suala hilo kwa kuwa bado halijafikishwa mahakamani, uchunguzi zaidi unaweza kuendelea.

Aidha, Masauni aliagiza Jeshi la Polisi kufanya kwa kina uchunguzi shirikishi na vyombo vingine dhidi ya askari wanaodaiwa na wananchi kuhusika kumpiga kijana huyo na kumsababisha kifo chake.

## Tanzania, China zaanzisha ushirikiano mafunzo na ujuzi

**Na Frank Monyo**

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Adolf Mkenda, amesema serikali kupitia Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT) imeanzisha programu ya ushirikiano na Taasisi ya Ufundi ya Chonqing (CQVIE) kutoka China ili kubadilishana uzoefu katika ujuzi wanaopata katika mafunzo ya kati.

Pia ameliagiza Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTVET) kuandaa semina na mafunzo ya kubadilisha uzoefu kila mwaka kati ya Tanzania na China ili kuendana na kasi ya mageuzi ya nne ya viwanda yanayohitaji ujuzi zaidi.

Prof. Mkenda aliyasema hayo jana baada ya kufungua semina ya kubadilishana uzoefu kwa viongozi wa vyuo vya elimu ya ufundi kutoka Tanzania na China iliyofanyika katika Chuo cha Uongozi cha Mwalimu Nyerere, Kibaha mkoani Pwani.

Alisema ushirikiano huo umekuja wakati muafaka Tanzania ikiwa katika mchakato wa mageuzi makubwa katika elimu.

"Tumeanzisha programu moja kati ya China na DIT. Digrii ya miaka minne wanafunzi wanachukuliwa mwaka wa kwanza wanasoma hapa Tanzania, miaka miwili wanasoma China, wanarudi Tanzania wanasoma mwaka mwingine mmoja inakuwa miaka minne.

Wanapata digrii ya hapa Tanzania wakiwa wamepata Diploma ya China," alisema.

"Kampuni ya Group Six wamesema wanafunzi hao wakimaliza wanaweza kutumika katika kazi zao bila wasiwasi wowote," alisema na kuongeza kuwa: Tumeanza na wanafunzi 30 ambao kwa sasa wapo mafunzo kwa vitendo.

Alisema lengo ni kuongeza idadi ya wanafunzi ili kufikia lengo na pia kutakuwa na nafasi ya wakufunzi kutoka China kuja kufundisha wakufunzi wa Tanzania.

"Sisi ndio tungependa tuchague vyuo hivi vya kati vya mafunzo ya amali ili kupata kile ambacho kitatusaidia kutoka hapa tulipo. China imeendelea kwa sababu ya kutoa mafunzo kwenye vyuo vya kati. Kuna wakati tulikuwa na kasi ya kila mmoja kuwa na elimu ya juu lakini kwa sasa mageuzi yetu ya elimu lazima yatoe mafunzo ya amali," alisisitiza.

Katibu Mtendaji wa NACTVET, Dk Adolf Rutayuga, alisema, semina hiyo imehusisha wadau wa vyuo 40 vya Tanzania na 30 vya China.

"Wezentu kutoka China wameendelea kwenye teknolojia hasa ya ujuzi, vijana kule wamekuwa chachu na msingi mzuri wa uchumi wa China, serikali yetu kuliona hilo wakatuagiza kuunganisha urafiki ili tubadilishane uzoefu.

"Tunataka vyuo vyote tuviunganishe na vya kule walimu na vijana wetu waende kule, na wao waje huku, ili vyuo vyetu vitoe vijana wenye ujuzi mahiri." Alisema.

Kwa mujibu wa Dk. Rutayuga, ujuzi kwa vijana utasaidia kutengeneza vitu vingi kwani vijana wa vyuo vya China wameunganishwa na viwanda ambapo vitu vinavyozalishwa vinaingia sokoni moja kwa moja.

# Simbachawene ataka viongozi kusikiliza kero ya watumishi

**Na Lusungu Helela,** MPWAPWA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, amewataka viongozi wa ngazi za wilaya na halmashauri nchini, kujenga utamaduni wa kusikiliza na kufanyia kazi malalamiko mbalimbali ya watumishi wa umma.

Amesema kiu yake na serikali kwa ujumla ni kuona watumishi wakifurahia kuwa watumishi wa wananchi.

Simbachawene alisema hayo jana wakati akizungumza na watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa mkoani Dodoma huku akibainisha kwamba anatambua watumishi wanakabiliwa na changamoto mbalimbali na hawana sehemu ya kuzisemea.

Alisema watumishi waliokata tamaa hawawezi kutoa huduma bora kwa wananchi huku akisisitiza kuwa hali hiyo imekuwa ikiwaumiza wananchi na kuifanya serikali iliyoko madarakani kuchukiwa kwa matatizo yao kutopatiwa ufumbuzi.

Waziri Simbachawene alisema anataka kuona watumishi wa umma wakipata stahiki zao lakini na wakati huo huo watekeleza majukumu yao ipasavyo.

Kutokana na hatua hiyo, Simbachawene aliwataka makatibu tawala wa wilaya nchini ambao ndio wakuu wa utumishi wa umma katika ngazi ya wilaya, kutekeleza majukumu yao kwa kusikiliza vilio na malalamiko ya watumishi walio chini yao.

"Watumishi waliochukia na wenye malalamiko hawawezi kuleta matokeo chanya ambayo Rais Samia Suluhu Hassan anakusudia, hivyo mkuu wa wilaya, mkurugenzi wa halmashauri na katibu tawala wa wilaya shughulikieni matatizo ya watumishi" amesisitiza Mhe. Simbachawene.

Aidha, Simbachawene alisema watumishi wa umma wanaokiuka misingi ya utumishi wa umma kama vile mfano ulevi kazini ni vizuri wakawa wanaonywa kabla ya kuadhibiwa ikizingatiwa sasa hivi waajiriwa wengi ni vijana, hivyo wanachohitaji ni malezi pekee.

Katika kusikiliza malalamiko ya watumishi, miongini mwa malalamiko yalitolewa kwa wingi na watumishi hao ni kucheleweа kulipwa malimbikizo yao ya mishahara, kupandishwa madaraja, kuchelewa kulipwa fedha za uhamisho pamoja na kubambikiwa mikopo.

Mkuu wa wilaya ya Mpwapwa, Sophia Kizigo, alisema yeye na timu yake chini ya Katibu Tawala wa Wilaya watajipanga kusikiliza malalamiko ya watumishi ili kuhakikisha watumishi wa Mpwapwa wanaifurahia kazi yao.

Aliwataka watumishi wa umma kuacha kukopa kwa kutumia mshahara wote hali inayoufanya utumishi wa umma kudharauliwa na kusababisha mtumishi kuishi maisha magumu

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tahadhari ya TCU madalali wa elimu ya juu izingatiwe

**TUME** ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) jana ilitangaza kufunguliwa kwa dirisha la udahili wa wanafunzi wa shahada ya kwanza kwa vyuo vya elimu ya juu. Kutangazwa kufunguliwa kwa dirisha hilo kumetokana na kutolewa kwa matokeo ya kidato cha sita wiki hii, hivyo kutoa nafasi kwa wanafunzi wenye sifa kuomba kozi mbalimbali katika taasisi za elimu ya juu nchini.

Licha ya TCU kutangaza kuanza kwa maombo ya udahili, tayari Bodi ya Mipo ya Elimu ya Juu (HESLB) hivi katibuni ilitangaza kuwa kuna ongezeko la wananfunzi watakaonufaika na mikopo hiyo sambamba na wale watakaopata ufadhili katika masomo ya sayansi kupitia Mfuko wa Rais Samia (Samia Scholarship Fund). Kwa maana hiyo, wale wenye sifa zinazostahili wanatarajia kunufaika na mikopo hiyo ili kujipatia elimu katika fani mbalimbali zitakazowanufaisha kwa Maisha ya baadaye katika ajira au kujiajiri.

Pamoja na kufunguliwa kwa dirisha hilo, TCU imeonya wanafunzi watarajiwa wa taasisi za elimu ya juu Pamoja na wazazi na walezi wao kuhusu kuwapo kwa kundi la watu, maarufu kama madalali ambao hutumia fusa kama hiyo kuwarubuni watu kuwa watawasaidia kupata nafasi.

Kama wahenga wasemavyo kwenye msafara wa mamba na kenge wamo, vivyo hivyo linapoibuka suala kama hilo, kuna watu hujipenyeza kwa madai ya kutoa msaada kumbe wanatumia fursa hiyo kufanya utapeli ili kujipatia fedha kutoka kwa wazazi na walezi wa wanafunzi.

TCU imeshaweka bayana kuwa maombi yote kwa ajili ya kuona nafasi za kujiunga na taasisi za elimu ya juu zinafanywa kwa njia ya mtandao. Kwa mantiki hiyo, wanafunzi, wazazi na walezi wanapaswa kuchukua tahadhari katika suala hilo.

Kwa maneno mengine wasikubali kurubunuiwa na baadhi ya watu kuwa wanaweza kuwasaidia, hivyo ili kutimiza azma hiyo, watoe fedha. Kwa mantiki hiyo, vijana wanaotaka kujiunga na vyuo vikuu, wenye sifa kulingana na fani husika, wafuate maelekezo ya serikali vinginevyo msemo kwamba wajinga ndio waliwao, unawahusu.

Mbali na kutafuta nafasi za kuiunga na shahada kama ilivyobainishwa na TCU, tahadhari nyingine inayopaswa kuchukuliwa na wanafunzi, wazazio na walezi ni kuhusu maombi ya mikopo ambayo pia mchakato hufanywa kwa njia ya mtandao.

Kama ilivyo katika maeneo mengine kujitokeza matapeli, kuna baadhi ya watu wanaweza kutumia mwanya wa kujifanya madalali wa mikopo kwa madai kwamba wanawasaidia kupata fursa hiyo kwa sababu wanafahamiana na maofisa wa bodi au serikali. Kwa mantiki hiyo, huu ni muda wa vijana na wazazi wao kuwa makini na makundi ya watu wanaoweza kujitokeza kuwa ni watu wa msaada kumbe ni watu wanaotumia fursa kama hizo kuwaibia watu. Tahadhari kabla ya hatari na majuto ni mjukuu.

Ili kuhakikisha hayo yote hayajitokezi, ni muhimu wahusika wakafuatilia taarifa mbalimbali za vyombo husika kama vile TCU na HESLB kuhusu vigezo na masharti ya kujiunga na vyuo Pamoja na upatikanaji wa mikopo.

Jambo lingine la muhimu kwa wanafunzi tarajiwa wa shahada za kwanza ni kuwa makini katika uchaguzi wa kozi watakazozisomea badala ya kukurupuka na kufuata mkumbo. Wanachopaswa ni kufahamu kozi wanazotaka kujiunga nazo zinaweza kuwasaidia nini katika maisha yao ya baadaye.

Baadhi ya wanafunzi katika miaka ya nyuma waliwahi kujiunga na vyuo katika kozi kadhaa kwa sababu marafiki zao au ndugu zao waliwahi kuzisomea au kushawishiwa kuwa ni nzuri. Ni vyema wanafunzi hawa wakajua kuwa hivi sasa kuna tatizo la ajira, hivyo wanapochagua kozi hizo watambue kuwa zitawasaidia baada ya kuhitimu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Uhaba wataalamu wa maabara shuleni ni kikwazo, waongezwe

Na Sabato Kasika

**KATIKA** kuboresha elimu, jitihada mbalimbali zimekuwa zikifanywa na serikali, ikiwamo ujenzi wa madarasa, majengo ya maabara, ununuaji wa madawati na mahitaji mengine ya muhimu shuleni.

Aidha, serikali imekuwa ikihamasisha wananchi kushiriki kikamilifu katika uboreshaji wa miundombinu ya shule, hasa kutokana na kwamba shule hizo ni zao.

Lengo la serikali kufanya hivyo, ni kutaka kuhakikisha inaboresha elimu, kuanzia mazingira ya kufundisha na kujifunza ili yawe rafiki kwa walimu na wanafunzi.

Hata hivyo, pamoja ba juhudi hizo, kuna kikwazo ambacho kinaweza kukwamisha juhudi za serikali za kuboreaha elimu, hasa kwa upande wa wataalamu wa maabara.

Inaelezwa kuwa sekondari za umma, baadhi hazina wataalam wa maabara, hali inayosababisha wanafunzi washindwe kujifunza masomo ya sayansi kwa vitendo. Kutokuwapo kwa wataalamu maabara kwenye baadhi ya shule kunaweza kuwa ni doa linalovuruga juhudi hizo za kuboresha elimu.

Upungufu huo wa wataalamu wa maabara (Laboratory Technician) kwenye baadhi ya sekondari za umma, unaweza kurudisha nyuma jitihada za mafunzo kwa vitendo licha ya kuwapo kwa maabara katika shule hizo.

Hili linaibuliwa na mwanafunzi wa kidato cha nne wa Shule ya Sekondari Abuu Juma iliopo Kivule jijini Dar es Salaam, Fatuma Ally ambaye anasema shule hiyo haina wataalamu wa maabara

**Inaelezwa kuwa sekondari za umma, baadhi hazina wataalam wa maabara, hali inayosababisha wanafunzi washindwe kujifunza masomo ya sayansi kwa vitendo. Kutokuwapo kwa wataalamu maabara kwenye baadhi ya shule kunaweza kuwa ni doa linalovuruga juhudi hizo za kuboresha elimu.**

Ni katika bunge la wananchi lililoandaliwa na vituo vya taarifa na maarifa vya Kivule na Majohe jijini Dar es Salaam hivi karibuni.

Bunge hilo liliratibiwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), kwa lengo kujadili bajeti kuu ya serikali ya mwaka 2023/2024 kama imezingatia mrengo wa kijinsia katika sekta mbalimbali.

Kwa mujibu wake, shule hiyo haina wataalamu wa maabara, inatumika walimu tu ambao kimsingi si wataalamu wa maabara hizo.

Ukosefu wa wataalamu wa maabara hizo ni kikwazo cha kupata wataalamu katika fani mbalimbali wa baadaye.

Upungufu huo kiukweli unarudisha nyuma jitihada za mafunzo kwa vitendo katika shule za sekondari licha ya kuwapo kwa maabara katika shule hizo.

Kikwazo hicho cha kukosa wataalamu wa kuendesha maabara hizo kikipatiwa ufumbuzi itakuwa ni rahisi wanafunzi kuelewa masomo ya sayansi kirahisi kuliko ilivyo sasa.

Lakini pia niwapongeze wanaojaribu kutumia maabara hizo ingawa hawana ujuzi, ila wanatamani wanafunzi wao wawe na uelewa wa masomo ya sayansi. Pamoja na hayo, ukweli unabaki palepale kwamba kutumia walimu wasio na ujuzi ni jambo ambalo linahitaji hatua za haraka ili kufanikisha azma ya kuwa na mafanikio kwenye elimu kwa vitendo.

Ni kweli serikali imekamilisha kuweka maabara katika shule za umma kwa asilimia kubwa, hivyo ni vyema ikaangalia jinsi itakavyo wezesha shule kuwa na wataalamu wa maabara hizo.

**SAFU**

## FIKRA MBADALA

# Mjadala wa Bandari sasa uishe tusonge mbele



Pascal Mayalla

MJADALA kuhusu uendeshaji wa bandari kwa njia ya ubia chini ya makubaliano ya serikali (IGA) una sura tatu ambazo ni kihalisia, kisiasa na kisheria.

Kihalisia, hapa nazungumzia ukweli ulivyo (material facts), yaani vitu vya ukweli na uhalisia vilivyosababisha Tanzania ikaribishe DP World kutusaidia kuendesha Bandari yetu. Ni halisi kwamba bandari yetu ndiyo eneo la kimkakati na rasilimali muhimu kwa nchi za Afrika Mashariki kuhudumia eneo la maziwa makuu.

Lakini Bandari yetu ya Dar es Salaam imeshindwa kutumia fursa hiyo kutokana na uwezo mdogo wa nchi yetu kiuchumi kuiimarisha kiuwezo wa uendeshaji na kimitaji. Kutokana na ukweli huo, serikali ikawa inatafuta mbia wa kimkakati (strategic partner) wa kuungana nayo ili kutusaidia kuboresha uendeshaji wa bandari yetu. Hapo ndipo akajitokeza mwekezaji DP World.

Baada ya kutokea uhitaji wa kusaidiwa, kitu cha kwanza kabla hujasaidiwa ni kuwapo kwa utashi wa kisiasa kukubali umeshindwa na unahitaji kusaidiwa.

Baada ya IGA ya DP World kuridhiwa na Bunge letu tukufu, wanasiasa wenye majina na ushawishi, wakubwa na wadogo, wazee kwa vijana, walumbana kwa hoja za kisiasa ama kuunga mkono hiyo IGA aa kuipinga. Wakati wa mjadala huo, kuunga mkono au kupinga, nilitoa ushauri wangu wa hoja za kisheria.

Kwa vile IGA ni suala la kisheria, na kwa nafasi yangu kama mwanasheria na wakili wa kujitegemea, niliweka hoja zangu mezani. Japo Bunge limeridhia DPW kuendesha bandari zetu, hayo ni makubaliano tu.

Tukithibitisha kuna matatizo, tunarekebisha mkataba wa HGA, kazi nzuri iendelee. Wanasheria nao wanajitokeza wakubwa kwa wadogo, vijana kwa wazee, wakiwemo manguli wabobezi na wabobevu. Wengine wakipinga mkataba huo kwa hoja za kisheria wakiwamo Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS) na wengine wakiunga mkono.

Kadri siku zinavyokwenda, watetezi wa mkataba huu kisheria wanazidi kujitokeza lakini kitu cha ajabu katika utetezi wao, hawajibu hoja za kisheria zilizoibuliwa kuipinga IGA hii.

Kutokana na kuwapo kwa vuta nikuvute katika jambo hili, ningependa nishauri ifuatavyo;-

Kwanza, mihilimili ya dola, yaani Bunge, Serikali na Mahakama si Mungu na si malaika kusema haikosei. Kwenye hili la IGA ya DPW, kuna uwezekano mkubwa serikali yetu inaweza kuwa imetukosea sana na Bunge letu tukufu nalo limetukosea sana kuiridhia bila kujiridhisha kwa kiwango cha juu.

Pili kwa vile Bunge, Serikali na Mahakama ni mihimili, ni kama baba ndani ya nyumba. Baba ambaye ni kichwa cha nyumba, anapokosea inakuwa aibu kwanza kukiri tu kosa na hata unapona umekosea na kutambua makosa yako, ni vigumu sana kuomba radhi au kuomba msamaha. Hivyo msitegemee kama serikali yetu au bunge litajitokeza na kukiri makosa kuhusu IGA hii.

Tatu, Inapotokea hali hiyo, baba mwenye nyumba amekosea, si lazima akiri makosa na kuomba msamaha lakini anapobaini amekosea, ana wajibu wa kurekebisha makosa kwa kufanya yaliyo sahihi.

Nne, kwenye hili la IGA ya bandari na DPW, siwezi kusema serikali yetu na bunge letu tukufu wamekosea. Nilichofanya ni kuonyesha makosa na matundu ya mahali panapovuja, hivyo ni jukumu la mwenye nyumba wetu kuziba hayo matundu. Ninachoomba toka kwa serikali yetu sikivu ni hoja zote za kisheria zilizoibuliwa na wanasheria mbalimbali, zijibiwe kisheria na si kisiasa.

Kwa vile hoja zote makini za kisheria kupinga IGA hii zimetolewa kwa maandishi zikiandamana na vifungu, nashauri serikali yetu, bunge letu na mahakama yetu kujibu hoja za kisheria, kwa majibu ya kisheria na si majibu ya kisiasa. Fani ya sheria ni fani bahari na mwanasheria yeyote anaweza kutoa hoja yoyote na kuongelea ndani ya bahari ya kisheria kwa kina chochote kwa kuwa anajua kuongelea.

Sita, nikiwa mwanasheria, katika hoja zangu "Japo Bunge Limeridhia, DPW Kuendesha Bandari Zetu, ni Makubaliano Tu. Tukithibisha Kuna Matatizo, Tunarekebisha Mkataba wa HGA, Kazi Nzuri Iendelee", nimeibua hoja moja kuu ya 'the capacity to contract' kwa Tanzania kama nchi, kuingia mikataba ya kimataifa na mtu ambaye hana uwezo kuingia mkataba (an international treaties with a person who has no capacity to contract). Hoja hii ijibiwe kikamilifu

Wakati nikiendelea kusubiri majibu ya kisheria kwa hoja zangu za kisheria kuhusu hii IGA, kwa sababu imeleta maneno maneno na kelele nyingi, nashauri uwapo wa uwazi mkubwa kabisa kwenye HGA ya Bandari ili mambo kama ya IGA ya Bandari na DPW yasije yakajirudia kwenye HGA.

Saba, naomba nimalizie kwa kuzungumzia kidogo kitu kinachoitwa karma. Licha ya kelele zote zinazopigwa kuhusu hii IGA ya DPW na Bandari, Bunge limeziba masikio kwa mkuu wa mhimili huu kutoa kauli za kujimwambafai, wakati serikali iko kimya bila kujibu hoja za kisheria zilizoibuliwa na watu na makundi mbalimbali wakiwemo TLS. Naliomba Bunge na serikali yetu kujibu hoja, huku nikiiomba mahakama kutenda haki.

Serikali yetu, bunge letu na mahakama zetu zina wajibu wa kuwatendea haki Watanzania. Wajibu huo si hisani (favour) bali ni haki. Natoa wito kwa bunge letu, serikali yetu na mahakama yetu, hata kwenye hili la DPW na serikali yetu, Watanzania tutendewe haki na Watanzania tusipowatendewa haki na vyombo hivi, the karma itafanya!

**Wasalaam**
**Paskali**
**+255 754 270403**

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Kumbe kukaa kimya nako ni kuongoza!



Na Joseph Kulangwa (kulangwasos@gmail.com)

**Lakini yakamfikia mwenye dhamana ya wizara yake ya afya, akamshangaa kigogo yule na kusema atafuatilia kadhia hiyo, kwa sababu taaluma hairuhusu kuoshya vyombo vya tiba kama hivyo.**

WENGI mnakumbuka usemi maarufu wa kiongozi mkuu wa China, Mao Ze Dong, kwamba 'No Research No Right To Speak?' Yaani usiseme kitu bila kuwa na uhakika nacho.

Lakini pia, inaweza kumaanisha kuwa usifanye jambo bila kuwa na uhakika nalo. Basi hivi karibuni usemi huo ukabanangwa na baadhi ya wakubwa zetu Bara na Visiwani katika kutekeleza majukumu yao.

Hapa Bara mnakumbuka yule bi mdogo aliyeonekana kwenye video akisafisha vifaa tiba vya hospitali ya Kivule, Ilala akitumia maji baridi ya bomba na mchanga?

Visiwani mnamkumbuka yule mkubwa wa Baraza la Sanaa aliyeibuka na kutoa tamko la kupiga marufuku wanaume au wavulana kusuka nywele huku akiwaambia atakaye kufanya hivyo, atatakiwa kununua kibali kwa Sh milioni moja!

Hakuishia hapo, akasema kama vipi basi Sh. mia itakuhusu kununulia wembe ili ukwangue kichwa na kubaki na uwaraza? Mnakunmbuka jinsi walivyoangukiwa na vitu vizito vichwani?

Haikupita siku baada ya matamko yao, wazito walio juu yao wakaibuka na kukanusha kilichosemwa na kufanyika. Ilala akaibuka mzito na kusema hapana sababu ya kushangaa yaliyofanywa na binti yule. Kigogo huyo akasema ulikuwa utaratibu wa kawaida kusafisha vifaa vilivyokaa stoo kwa muda.

Lakini yakamfikia mwenye dhamana ya wizara yake ya afya, akamshangaa kigogo yule na kusema atafuatilia kadhia hiyo, kwa sababu taaluma hairuhusu kuosha vyombo vya tiba kama hivyo.

Hata hivyo, aliyesema ni jambo la kawaida kabisa akahamishia hasira zake kwa mdogo wake na kumsimamisha kazi kwa kuacha kibinti kile kisugue vifaa tiba kwa mchanga.

Zanzibar nako mambo hayakuwa shwari, akaibuka naye mwenye dhamana ya sanaa, mila na utamaduni akakanusha kabisa yaliyotamkwa na mdogo wake, akasema yawezekana ni ulimi kuteleza.

Kwa kweli ikawa ni wiki ya ndimi kuteleza Ilala na Unguja. Ula usemi wa Mao ukadhihiri kabisa kwamba bila utafiti acha kufunua kinywa au kunyoosha mikono kutenda jambo bila uhakika.

Hizi ni hulka za baadhi ya viongozi ambao wakikaa kimya kwa muda mrefu hutaka waibuke waseme au watende, na kuonekana wapo na wanafanya kazi, lakini kumbe wanaharibu na kupotosha jamii, na kwa kweli mitandao isingekuwapo, vifaa tiba vile vingeendelea kusuguliwa kwa mchanga na kuoshwa kwa maji baridi na kuanikwa juani. Na ndiyo sababu Waziri mwenye dhamana akaibuka na kupongeza mitandao ya kijamii.

Hakuishia hapo, akawataka wananchi wapatapo taarifa kama hizo mara moja watoe ushirikiano kwa wenye mamlaka, ili hatua stahiki zichukuliwe kwa maslahi mapana ya umma.

Hivi nani alisema bakteria wanaweza kufa kwa kusuguliwa na mchanga na kumwagiwa maji baridi na kuanikwa juani? Kama si kuendelea kuhatarisha maisha ya wagonjwa ni nini basi?

Yule kigogo aliyeibuka baada ya video ile na kusema ni utaratibu wa kawaida, sidhani kama ameachwa aendelee na nafasi yake ile, baada ya yeye kukimbilia kumchukulia hatua kiongozi wa hospitali ile.

Alitakiwa kutulia na kuiangalia ile video na kuchanganya na taaluma yake, na kuchukua hatua kabla Waziri hajaiona na kuchukua hatua, huo ndio udhaifu aliotuonesha na anastahili kubanwa pia.

Kama ataendelea na majukumu yake kama kawaida, basi naye amfungulie kifungo mganga yule aliyemweka pembeni akisubiri uchunguzi wa kitu gani sijui! Akibanwa litakuwa funzo na atakumbuka usemi wa Mao.

Hali kadhalika ndugu yetu wa Unguja, naye asiishie kutelezesha ulimi kwani naye anastahili kibano kutokana na taharuki aliyosababisha kwa vijana wanaoona ni bora kusuka kuliko kunyoa. Ndugu zangu marasta na Wamasai sijui wangekimbilia wapi masikini!

Viongozi wetu kukaa kimya nako ni kuongoza, si lazima utoke hadharani na kutoa matamko yanayoibua taharuki kwa wananchi kama ilivyotokea Kivule na Unguja. Acheni kazi iendelee.

**Alamsiki!**

# Mwongozo mpya kubaini vikwazo katika elimu

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

SERIKALI kwa kushirikiana na Programu ya Shule Bora imekamilisha mwongozo mpya wa kitaifa wa kubaini na kushughulikia vikwazo vinavyokwamisha utoaji wa elimu jumuishi kwa watoto wote nchini.

Kwa mujibu wa ripoti ya Juni, mwaka huu iliyotolewa na Programu ya Shule Bora na kusambazwa kwa vyombo vya habari, mwongozo huo utasaidia utekelezaji wa Kiashiria cha Ufanisi (DLI) kupitia programu ya EpforR.

Ripoti hiyo imeeleza kuwa mafanikio ya kiashiria hicho yataiwezesha serikali kutoka kwa wafadhili ambao ni Global Partnership for Education (GPE) Dola za Kimarekani 2,612,400.00 ambazo zitasaidia kugharamia shughuli za elimu nchini.

Aidha,mafunzo endelevu ya walimu kazini yameanza kutokea ili kuboresha ujuzi wa walimu, kujenga uwezo wa kujiamini, kutoa motisha na kusaidia ustawi na maendeleo ya watoto.

Baada ya kuanzishwa kwa mfumo huo katika shule za msingi, halmashauri tano za mkoa wa Singida zimefurahishwa na mafanikio ya shule bora ya kutumia mbinu ya mafunzo endelevu ya walimu kazini na sasa imeanza kutumika katika shule za sekondari mkoani humo.

Katika hatua nyingine, halmashauri zimeanza kuchapisha jarida la Shule Bora kwenye mikoa inayotekeleza programu ya Shule Bora. Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji mkoani Pwani ndiyo inayoongoza kwa kutekeleza mpango huo.

Chapisho hilo ni matokeo ya mafunzo yaliyotolewa kwa maafisa habari katika mwaka wa kwanza wa programu ambapo kitini cha jarida la Shule Bora kiliandaliwa ili kurahisisha mchakato wa uandaaji wa majarida kwa kukusanya taarifa na kutangaza mafanikio ya sekta ya elimu kwa umma.

"Halmashauri zinaweza pia kutumia majarida hayo kutoa taarifa za masuala ya elimu kwenye mikoa yao, kubadilishana mbinu bora za ufundishaji na ujifunzaji na kukuza utamaduni endelevu wa kufanya maboresho," imeeleza ripoti hiyo.

Aidha, ripoti hiyo imeeleza shughuli zinazotarajiwa kutekelezwa Julai, 2023 kuwa ni uwasilishaji wa mpango kazi wa mwaka wa pili kwa wadau ngazi ya mikoa na halmashauri na kufanya mapitio na kuhakiki utendaji wa viashiria vya ufanisi vya EPforR mwaka 2023.


Shughuli zingine zitakazofanyika ni kukamilisha vipindi vya redio vya kuhamasisha mabadiliko ya tabia ya kijamii vinavyolenga kukuza elimu bora na jumuishi na kuandaa mwongozo wa ugawaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia (vitabu) kwa shule za sekondari (S-TLMAP).




Wafanyakazi wa kampuni ya usafi wakizoa takataka bila ya kuvaa vifaa vya kujikinga mikononi katika eneo la Mawasiliano, Dar es Salaam mapema wiki hii, kitendo kinachoweza kuhatarisha afya zao. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Aisha atoweka kwao akitokea madrasa

**Na Pilly Kigome**



MWANAFUNZI wa Kidato cha Kwanza, Aisha Ezekiel Mahogwa (14) wa Shule ya Sekondari Kimaseki, Arusha, anatafutwa na wazazi wake baada ya kuondoka nyumbani kwenda madrasa na kutorudi tena.

Akizungumza katika ofisi za gazeti hili juzi, mama mdogo wa mwanafunzi huyo, Edina Joel, mkazi wa Gongo la Mboto, Dar es Salaam, alisema mtoto huyo aliondoka nyumbani Juni 9, mwaka huu, majira ya jioni kuwa anakwenda madrasa.

Alisema Aisha alitoka nyumbani na wadogo zake wawili na msaidizi wa ndani kwenda madrasa na wakati wakirejea, aliwaambia wadogo zake kuwa watangulie nyumbani kwani yeye kuna sehemu anakwenda aliagizwa nguo na mama yao.

Baba mzazi wa mwanafunzi huyo, Ezekiel Mahogwa, akizungumza kwa njia ya simu kutoka Arusha, alisema baada ya tukio hilo walitoa taarifa katika Kituo cha Polisi cha Kijenge Arusha na kupatiwa RB KJ/RB/931/2023.

Alisema mara ya mwisho mtoto wao wakati akitoka nyumbani alikuwa amevaa gauni yenye rangi ya maziwa na hijabu ya rangi nyekundu.

Aliomba kwa taarifa yeyote atakayemwona apige simu 0686 506071, 0686 402982, 0784993045 au awasiliane na kituo chochote cha polisi.

# Polisi yachunguza mwili uliokutwa kwenye gari

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, limesema linachunguza tukio la mauaji ya mkazi wa Kimara Temboni mkoani Dar es Salaam, Josephat Mgeni (47).

Mwili wa mgeni ulikutwa kwenye gari huku ukiwa na jeraha kubwa kichwani.

Kamanda wa Kanda hiyo, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Jumanne Muliro, aliyasema hayo juzi kupitia taarifa yake kwa vyombo vya habari, akisema uchunguzi huo unahusisha pia, baadhi ya vitu vilivyokutwa eneo la tukio vingine vikiwa ni vya jinsia ya kike.

Alisema tukio hilo lilitokea usiku wa manani wa kuamkia jana maeneo ya Mbezi Luis, Wilaya ya Ubungo na mtu huyo anadaiwa kuuawa.

"Mwili wa marehemu umekutwa kwenye gari namba T 552 DMB aina ya Toyota RAV4 huku ukiwa na jeraha kubwa kichwani. Polisi inaendelea na uchunguzi ikiwa ni pamoja na kuchunguza vitu vilivyokutwa eneo la tukio," alisema.

Alisema mwili wa marehemu umehifadhiwa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH) Tawi la Mlongazira kwa uchunguzi zaidi na hatua zaidi za kisheria zitachukuliwa baada ya upelelezi wa kina.

# Wajasiriamali wawezeshwa mil. 10/- kukuza biashara

**Na Mary Geofrey**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, kwa kushirikiana na Taasisi ya Lalji Foundation, wametoa msaada wa Sh. milioni 10 kwa ajili ya kukuza mitaji kwa wajasiriamali wadogo 50 wanaojihusisha na uuzaji wa samaki, vyakula na vinywaji.

Msaada huo uliotolewa Kata ya Kivukoni na kila mjasiriamali amekabidhiwa Sh. 200, 000 ili kuinua biashara wanazofanya.

Akizungumza juzi jijini Dar es Salaam wakati akikabidhi msaada huo kwa wajasiriamali hao, Chalamila aliwataka kutumia fedha hizo kuinua mitaji na kuleta mabadiliko ya kiuchumi kwa kukuza biashara.

"Fedha hizi zikatumike katika matumizi yaliyo shahihi.

Tunajua mna shida ya mitaji na mmekuwa mkikopa mikopo umiza kutoka katika taasisi za kifedha na kujikuta mkilipa kila siku na wengine kushindwa.

"Msiwe mnakopa kila taasisi ya kifedha inayokuja kwako, muwe mnakopa kwa starа na isiyoumiza," aliwaonya.

Alisema wako ambao wamechukua mikopo kwa lengo la kujiendeleza kibiashara kutoka taasisi mbalimbali za kifedha, lakini biashara zinapowashinda wanakimbilia ofisini kuomba msaada.

Mkurugenzi wa Lalji Foundation, Imtiaz Lalji, alisema walitembelea katika soko la Kivukoni na kubaini wajasiriamali wanahitaji msaada wa kifedha ili wajiendeleze kiuchumi kwa kukuza biashara hizo.

"Hii ni taasisi ya kifamilia ambayo tumezaliwa nchini, lakini wengine wapo nchi zingine na kwa pamoja tumeona kile tunachokipata tusaidie wengine wenye uhitaji katika makundi mbalimbali ndani ya jamii yetu.

"Tayari tumeshasaidia wenye matatizo ya macho 348 katika hospitali ya Kahama, lakini pia tulishatoa futari kwa watu 200 wakati wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani," alisema.

Mmoja wa wanufaika wa msaada huo, Rahilu Nyundo, alishukuru na kusema fedha hizo zitasaidia kukuza biashara zake.

# MAISHA

JULAI 16, 2023

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*

Ukurasa 14




**JUISI YA NANASI...**

## MAISHA NI NYUMBA


Ukurasa 15






## KATUNIKA


Ukurasa 16



# MWANZO WA UCHUMBA

Ukurasa 12


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA



| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| C | C | P | E | N | B |
| H | A | X | B | U | U |
| A | W | Y | O | O | I |
| L | I | J | O | J | N |
| K | B | P | K | O | K |
| R | U | L | E | R | R |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| A | ■ | U | S | I | K | U |
| S | ■ | ■ | ■ | L | ■ | C |
| U | ■ | Y | A | I | ■ | H |
| B | A | A | ■ | P | U | A |
| U | ■ | N | A | O | ■ | C |
| H | ■ | G | ■ | ■ | ■ | H |
| I | F | U | T | E | ■ | U |


## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:


MIA, TII, UFA, WAO, KINDA, ASALI, NJIWA, TAMBA, TAFUTWA, ASHONWE

## TOA TOFAUTI 5




## AMSHA AKILI

WAONESHE MAKINDA HAYA NJIA YA KUTOKA KIOTANI.



## WATOTO

# PAKA RANGI



@ A.MSAMBA

## CHEKA

JAMAA mmoja ambaye ni mara ya kwanza kutembelea mjini, aliwaacha watu hoi kwa kicheko baada ya kupelekwa katika kibanda cha kununulia koni.

**Mama:** Ebu nipatie koni mbili ya kwangu na huyu ndugu yangu

**Jamaa:** Duu, chakula gani hiki mbona kama konokono wa kule shambani, ila huyu ana rangi nzuri

**Mama:** Hapana hii ni koni

**Jamaa:** Tafadhali mama siwezi kula, bora uninunulie togwa

**Mama:** Sema taratibu unanitia aibu.

**SWALI**

Tabia za binadamu zinakaribiana na mnyama gani wa porini?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Wanayopaswa kujua mawifi na mashemeji

KARIBU tena msomaji wangu tuendelee na mada zetu katika duru la Maisha Ndivyo Yalivyo. Tumekuwa tukijadili mfululizo kuhusu jinsi ya kuishi na mama mkwe. Na wiki iliyopita niliahidi kuwagusa mawifi na mashemeji.

Wiki iliyopita nilitaja mambo kadhaa ambayo binti aliyeolewa anapaswa kuzingatia ili aweze kuishi na mama mkwe muda mrefu. Wapo waliojifanya wababe wakajikuta mapema wanazikimbia nyumba zao wenyewe.

Wengine wakajikuta wanapoteza hata maisha baada ya wakwe zao kuwafanyia vurugu mbalimbali. Unapokwenda kwenye miji ya watu, unapaswa kuwa mtulivu na kusoma mazingira ili mwisho wa siku uweze kuendana nao. Ukifanya vile utakavyo wewe, utakwama!

Leo niangazie mawifi na mashemeji. Kila wifi au shemeji anatakiwa kuwa makini na mke wa kaka yake, huku ukiweka akilini kwamba chochote utakachopanda ndicho utakachovuna.

Hivyo, kama wifi na shemeji unapaswa kuishi kwa hekima. Kama ndoa ya kaka yako ikivunjika kwa sababu yako, Mungu atakuadhibu. Alichokiunganisha Mungu, shemeji au wifi hapaswi kukitenganisha.

Ushauri wa kuzingatia ni kwamba; jifunze kumkubali wifi au shemeji yako kama sehemu ya familia yenu tokea siku ya kwanza ya kumfahamu.

Pia usijenge tabia ya kumsema wifi yako kwa wazazi wenu. Jifunze kuongea tofauti zenu bila hata kutoa taarifa kwa kaka yenu. Kumbuka siku zote kuwa mke wa kaka yako ni rafiki yake wa karibu, na siyo wewe.

Usipende kufuatilia sana nini kinachoendelea kati yao, wewe jali mambo yako. Kama kuna tatizo limetokea kati yao, jaribu kuwatuliza na siyo kuwaongezea matatizo. Chochote utakachofanya Mungu atakuhukumu.

Kwa maombi makali jifunze kupuuzia makosa yake na msamehe mapema iwezekanavyo. Usije ukamsema au kumsengenya, wala kumsemea uongo au kuongea maneno mabaya juu yake.

Hata Mungu anasema katika moja ya neno lake, kwamba, "wasimtukane mtu yeyote, wasiwe wagomvi, wawe wema, wakionyesha upole wote kwa watu wote" (Tito 3:2).

Kwa mantiki hiyo, usipende kufanya nyumba yao kuwa uwanja wa vita kwa kila mapungufu yanayotokea kwa wifi/shemeji yako. Uwe mtu anayependa kutunza amani na siyo kuvunja ndoa yao.

Epuka pia kujishughulisha na mambo ambayo yanaweza yakawafanya kukosa maelewano. Utaheshimika pale utakapoishi mbali nao na usipende kuishi kwenye nyumba yao! Kwa kufanya hivyo utakuwa umejenga urafiki baina yao.

Usikubali kuishi nao labda kwa sababu ambazo hazizuiliki. Usitarajie mambo makubwa kutoka kwa kaka yako na mke wake, kwani ndio kwanza wameoana na wana majukumu mengi.

Epuka kumuonea wivu wifi/shemeji yako, badala yake mpongeze na muonyeshe upendo. Jifunze kusamehe na kusahau. Heshima lazima itawale. Jifunze kumheshimu wifi/shemeji yako na wewe watakuheshimu.

Kingine, fahamu kuwa wewe siyo msimamizi wa jiko lake na kwamba huruhusiwi kabisa kuingia chumbani kwao, na kama umealikwa kuingia, bisha hodi kabla hujangia.

Mawifi wengine wanapoingia kwenye nyumba ya kaka yao, hudiriki hata kuingia chumbani eti kukagua kama mke wake ni msafi au la. Hii siyo sawa. Elewa ya kuwa chumbani ni faragha ya wanandoa na siyo kila mtu anapaswa kuingia.

Jifunze kutoa ulicho nacho siyo kupokea tu. Msaidie wifi yako kazi za jikoni, usimuache afanye kazi zote za nyumbani kwani yeye siyo mtumwa wala mfanyakazi!

Katika eneo hili, wapo mawifi wanapokuja kumtembelea mke wa kaka yao hujifanya maalumu na kukaa tu wakisubiri wahudumiwe. Eti ni wageni na wamekuja kwa kaka yao. Matokeo yake wanakaa kusubiri wahudumiwe kwa kupikiwa na hata kuandaliwa mezani.

Hili ni kosa. Unapokuja kwa wifi yake unapaswa kuchangamka na kuwa karibu naye huku ukimuuliza eneo gani la kumsaidia kumpunguzia mzigo wa kazi. Kama ni jikoni ingia msaidie kazi iliyopo ili kukamilisha shughuli zote mapema. Huo ndio upendo.

Penda watoto wa kaka yako na wahudumie ili kuonyesha unawajali.

Usije ukachukua nafasi ya kutokuelewana nao kumuangusha wifi/shemeji yako. Usiingie majaribuni kwa kutaka kusimamia jiko lake, usije ukapigwa na Mungu.

Mpenzi msomaji, bila shaka umejifunza jambo kuhusu mawifi na mashemeji wanapokuwa katika miji ya kaka yao.

***Wiki ijayo nitamalizia jinsi mke anapaswa kuchukuliana na mawifi na mashemeji zake. Je, una maoni, kisa? Ujumbe mfupi 0715268581.***

## WARAKA WA NDANI
Na Godfrey Mushi



# Aweso pitia Arumeru kuna shida mahali

Wakati wa shida, maisha yanatufundisha kuchagua utu badala ya kudhalilisha, kupaza sauti, wakati wa dhuluma na kusamehe badala ya chuki. Ndiyo!

Wakati huu ambao kuna wananchi wenzetu hawana maji ya bomba kwa miaka 48 sasa, kuna wengine wanayatumia vibaya hadi mamlaka kulalamika. Huko ndiko kunaamsha hasira ya wale wasiofikiwa na neema hiyo.

Mathalani, adha ya kukosa maji wananchi wa kijiji cha Karangai, kilichoko Kata ya Kikwe, wilaya ya Arumeru mkoani Arusha, imesababisha wakazi wake wengi kuugua na kulazwa hospitalini kutokana na tishio la magonjwa ya amoeba, kichocho, typhoid na kuhara.

Wananchi hao hawana huduma hiyo ya maji safi na salama tangu mwaka 1975 na kwa sasa wanahemea maji machafu yanayotiririka kutoka kwenye mashamba ya mpunga ya Manyata.

Kero hii ya maji, si tu imeathiri wanawake kwa kutumia muda mwingi kutafuta maji kwa matumizi ya nyumbani, badala ya kuzalisha mali bali sekta za elimu, afya na shughuli za kimaendeleo.

Si kwamba Arumeru ina tatizo la kijiolojia, ndio maana inakabiliwa na uhaba wa vyanzo vya maji vya kudumu, au maji hupatikana umbali mrefu, la hasha!

Ni suala la utashi wa viongozi wetu. Hawajataka kuielekeza akili yao na rasilimali fedha za serikali kutatua tatizo, hata pale yanapopatika hudumu kwa muda na hukauka.

Ukiwasikiliza wananchi wa Karangai, utaona wanavyoumizwa na hilo, na wanaona tatizo lao linaweza kupata ufumbuzi wa kudumu, iwapo serikali itawekeza fedha za kutosha kujenga mradi mpya wa maji.

Hicho kijiji kwa ujumla, kinakabiliwa na changamoto mbili kubwa, maji na umeme.

Mosi, madai yao ni kwamba, maji ambayo wanakunywa ni machafu, na kibaya zaidi hawana msemaji wa kuwasemea.

Kwa sababu viongozi wao kila mwaka wamekuwa wakiwaahidi na kuwageuza mtaji wa kura, wakati uchaguzi unapofika.

Nimemnukuu mmoja wa wakazi hao akisema kuna wananchi wengi wako hospitalini wakitafuta tiba kutokana na kunywa maji machafu na wengine wameshafariki kwa ajili ya magonjwa yanatokana na kunywa maji machafu.

Maji hayo ni yale yanatoka kwenye mashamba ya watu ya mpunga kutoka Usa River na yanapotiririka kwenda eneo hilo, ndio wakazi wa Karangai wanayatumia kwa ajili ya kunywa.

Kwamba, maji yanayotumika kunywa ni maji ya umwagiliaji, na siyo maji yanayofaa kwa ajili ya matumizi ya binadamu.

Lakini kinachowasikitisha zaidi, maji yametoka Rundugai, Wilaya ya Hai, Mkoa wa Kilimanjaro, yamepita Kijiji cha Karangai kwenda Jiji la Arusha, lakini wao hawana maji.

Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Wilaya ya Arumeru, inakiri ni kweli huduma ya maji katika kijiji cha Karangai, haijafika kwenye vitongoji vyote ila yameishia Kitongoji cha Bondeni.

Katika majibu yake, anasisitiza kwamba mpango wa serikali kwenye bajeti ya mwaka huu wa fedha 2023/24 ni kuusogeza Mradi wa Maji kutoka Bondeni hadi Miembeni ambako wananchi hawana hiyo huduma ya maji.

Ni matarajio yetu hadi kufikia mwezi wa tisa mwaka huu kitongoji hicho kitakuwa kimefikiwa na Huduma ya maji."

Hata kama mikakati hiyo ya serikali inaweka picha za matumaini kwa wakazi hao, hata hivyo swali linabaki ni lini utekelezaji huo utakamilika?

Je, katika kipindi hicho chote wananchi hao watatumia vyanzo gani vya majisafi na salama ili kujiepusha na magonjwa ya tumbo na kutumia muda wao vyema katika uzalishaji?

Wananchi wengi wanaitupia mzigo RUWASA kwa kushindwa kutatua kero yao.

Hata hivyo, wengi hawajui kuwa kiwango cha bajeti kinachopangwa kutokana na mapato ya serikali kwa ajili ya kutatua tatizo hilo, wakati tatizo linaendelea kuwa kubwa mwaka hadi mwaka.


Kiukweli yanapokosekana maji yanaathiri shughuli nyingi za maendeleo, hivyo ni vyema sasa serikali kwa maana ya RUWASA, wakaangalia uwezekano wa kuongeza bajeti ya maji.

Na ninyi watoa maamuzi hakikisheni mnapigania ongezeko la bajeti ya maji ili kuwaondolea wananchi kero ya kusaka maji katika umbali mrefu.

***•Godfrey Mushi ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa simu namba 0715 545 490 au barua pepe: ghandsome79@gmail.com***

# HARUSI





Baada ya kuvishana pete ya uchumba je mnataka kupata picha ya kumbukumbu? Pichani ni baadhi ya mitindo ya kufurahisha ya namna ya kupiga picha zinazowapa furaha. PICHA: PINTEREST





# MITINDO





# ‘ROLL NECK’

## Ni habari yote

ROLL Neck vazi hili lilianza kutumika miaka ya 1970, lakini hadi sasa limekuwa likipendwa na watu wa rika mbalimbali na hasa vijana.

Fulana hizi zenye shingo ndefu zinaendelea kuboreshwa kila wakati kutokana na kuwa na mwonekano mzuri pale mtu anapovaa.

Ni vazi la kipekee ambalo unaweza kuvaa peke yake au kuweka tabaka lingine la nguo bila kupoteza mwonekano wake.

Kimsingi linapendeza zaidi kuvaliwa nyakati za jioni au kipindi cha baridi, kutokana na kuwa na sifa ya kuhifadhi joto

Roll Neck, unaweza kudhani ni vazi la kitajiri, lakini kila mtu anaweza kuvaa kulingana kipato chake.

Unapovaa fulana ya aina hii, unaweza kubadilisha kabisa hisia za jumla ya mkusanyiko wa kimuonekano, hasa kwa kuzingatia ushonaji wake mkali.


Inapendeza sana kama itavaliwa chini na jeans au suaruali ya kawaida inayobana kiasi.

Itapendaza zaidi kama fulana ya aina hii ukatupia ndani ya koti na kuachia eneo la mbele likiwa wazi na kuonekana vyema fulana.

Kuanzia safu za wikendi hadi ushonaji wa siku ya kazi, hapa kuna njia nane zisizo salama za kutikisa vazi linaloleta mabadiliko zaidi msimu huu.

UREMBO

Na Mary Geofrey



# NGOZI LAINI

MSIMU wa kipukwe umeshika kasi katika maeneo mengi nchini, sio jambo la ajabu kuona watu wamevalia makoti na majaketi kujiongezea joto la mwili kutokana na hali ya baridi na upepo.

Mambo haya tulizoea kuyaona katika miji yenye baridi kali kama Arusha, Moshi, Njombe.

Ila sasa hali hii ipo Dar es Salaam na maeneo mengi, ni vizuri ukajua nini ufanye ili ujiweke sawa wakati huu.

Changamoto kubwa ni baridi na upepo ambao unasababisha ukavu wa ngozi wa hali ya juu wengine inafikia hadi kukatika midomo na miguu na maeneo mengine.

Fanya haya kuondolea ukavu wa ngozi.

Jambo kubwa kunywa maji ya kutosha.

Wakati huu sio wa kunywa maji kwa sababu ya hali ya hewa ila njia yenye matokeo chanya ni kujitahidi kunywa maji yako pia unaweza kuongeza limau au kununua maji yenye ladha tofauti

Subiri ngozi ikauke baada ya kupaka mafuta

Kama ndio kwanza umetoka kupaka mafuta yako kama ni losheni au mafuta mengine subiri kidogo ngozi ikauke kabla ya kutoka ndani.

Kwa sababu ukitoka ndani ngozi bado ina unyevu ni wazi kuwa ukipigwa na upepo itakauka haraka na kupauka sana.

**Itaendelea wiki ijayo......**





MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Juisi ya Nanasi, Karoti na Tangawizi

TUNDA la nanasi na karoti vinachangia sana sukari yote ambayo juisi inatakiwa iwenayo.

Tangawizi inaweka uwiano sawa wa ladha kati ya nanasi na karoti, kama sio mpenzi wa tangawizi sio lazima kuitumia.

Lakini kama ni mpenzi wa nanasi au karoti unaweza kuzidisha kimojawapo ili upate ladha halisi ya unachokipenda.

Tangawizi Inategemea na ubora wa tangawizi, unaweza kuhitaji nyingi zaidi au wastani cha msingi uweze kupata harufu na ladha katika juisi yako.

Namna ya kuandaa

Safisha matunda yako na maji ya safu ya uvuguvugu na kisha anza kuyamenya kwa kutumia kisu kisafi na chombo safi cha kuwekea.

Changanya matunda yako kadiri ya uhitaji wako, kama nanasi lizidi au karoti na saizi ya tangawizi.

Ukishandaa weka kwenye blenda na anza kuyasaga yakilainika uanze kuchuja.

Juisi yako itakuwa tayati kunywa bila kuongeza sukari kwa sababu nanasi na karoti yana sukari za kutosha na kama utapendelea kuongeza utafanya hivyo.



MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**



# Chumba cha kulala nacho kinahitaji unadhifu

UMARIDADI huficha umasikini. Huo ni msemo ambapo , msemo huo umekuwa ukitumiwa na wahenga kuonyesha umuhimu wa mtu kuwa maridadi au nadhifu kila wakati.

Umaridadi ambao tumeuzoea sana ni ule wa umahiri wa kujiweka safi katika uvaaji au kwa lugha ya kigeni 'smart' wakati wote bila kujali una kipato kikubwa au la.

Lakini leo nataka nikwambie kwamba mbali na umahiri wa kujiweka safi katika mwili lakini pia unaweza kufanywa hata katika nyumba hususani katika chuma cha kulala.

Asilimia kubwa tumejikuta kukikifanya chumba cha kulala kama sehemu ya kurundika vitu ovyo eti kwa sababu hapaonekani katika uso wa wageni kama ilivyo katika sebule.

Kuna vitu muhimu ambavyo vinapaswa kuzingatiwa ndani ya chumba ili kukifanya kiwe na mvuto, chenye afya na hata kuimarisha ustawi wa nyumba yako ikiwamo mpangilio wake kwanza.

Hakikisha chumba chako kinawekwa katika mpangilio unaovutia hasa kwa kuangalia ukubwa na namna kilivyotengenezwa na hakikisha unajenga umbo katika kichwa chako namna unavyotaka vitu vyako vipangiliwe, na kuepuka kupanga vitu ilimradi.

Zingatia kuweka vitu ambavyo ni muhimu na vina kazi katika chumba chako na si kuweka kila kitu kwa sababu ukiweka vitu vingi ambavyo havina umuhimu kwanza chumba chako kitakosa hewa, kitakuwa na hewa nzito lakini pia kitapoteza mvuto.

Chumba kinachokosa mpangilio mzuri au kujazwa vitu pasipo sababu, uwezekano wa kukifanyia usafi wa uhakika ni mdogo na kwa maana hiyo hatari ya kuhifadhi wadudu ni kubwa.

Hakikisha fanicha muhimu pekee ndio zinawekwa ndani kwa mfano kitanda, kabati na 'dressing table' na kuhakikisha vinafanyiwa usafi mara kwa mara.

Kwa kitanda, zingatia kukifanyia usafi kila siku, si kutandika mashuka tu lakini kuhakikisha unakikagua kila eneo na kufuta kabla ya kutandika shuka zako.

Safisha kuanzia uvunguni, katika kila kona ya maungio yake na baada ya kujiridhisha kwamba umesafisha kila mahali bila kusahau kukagua chandarua kama kiko katika hali ya usafi, kukichomoa kwenye kitanda na kasha kutandika shuka zako.

Kumbuka kwamba inavutia zaidi na kukifanya chumba kionekane chenye mvuto zaidi unapotandika kitanda chako kwa kukilembesha kidogo. Usikubali kukiweka kikavukikavu na unaweza kutumia shuka zako hizo unazozitumia kwa siku husika na hata kwa kutumia mito.

Kwa upande wa kabati, nalo vitu vinavyowekwa ndani yake vinatakiwa vipangiliwe vizuri, ili liwe 'smart' na lisiharibu mpangilio wa chumba.

Hakikisha nguo zako unazipangilia vizuri katika sehemu yake, na viatu sehemu yake kwa kabati zenye sehemu ya kuwekea viatu hivyo.

Suala si kupangilia tu bali pia kabati linapaswa kusafishwa ili lisipate 'ukungu' na kuharibu nguo zako na mwisho wa siku ukasababisha harufu kwenye nguo.

Kwa upande wa 'dressing table', nayo vile vile inahitaji kuwa katika mpangilio mzuri, hakikisa vitu vinavyowekwa kwayo vinakuwa katika mpangilio mzuri ambao nao huvutia ukiwekwa vizuri. Ondoa kila kitu ambacho hakistahili kuweka hapo.

# Furahia holda za mawe kuwekea taa

**Na Restuta James**

MWEZI uliopita nilikuletea makala moja iliyokuwa inaeleza kuhusu matumizi ya vitu asilia yanavyoendelea kuleta mageuzi kwenye mapambo ya ndani.

Katika makala hiyo tuliona namna ambavyo mawe yanatumika kutengeneza masinki ya jikoni na kunawia mikono, na namna yanavyoweza kubadili mwonekano wa nyumba.

Hata hivyo, mageuzi hayo hayajaishia kwenye masinki tu kwani yamefika hadi kwenye vifaa vya umeme.

Mtaalamu wa umeme, Johnson Ngowi, anasema ziko 'holder' za taa zilizotengenezwa kwa mawe halisi na kunakishiwa ili kuzipa mwonekano wa kuvutia.

"Kama unavyoona, haya ni mawe halisi yaliyobuniwa na kunakishiwa kupata lamp holder unayoiona. Ni nzuri na zinatumika kama pambo ndani ya nyumba," anasema.

Ngowi anasema aina hiyo ya holder huwezi kuiweka kila mahali kutokana na mwonekano wake.


Anasema, zinapendeza zaidi kwenye kibaraza, ukuta wa koridoni na meza ya console.

Anasema taa hizi zinapendeza zikiwekwa kwenye ukuta wa pembeni na sio juu (kwenye dari).

Anasema: "Holder yenyewe tu ni pambo hata bila kuwasha taa. Inaongeza nakshi ndani ya nyumba na kukupa utulivu."



# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2023
SMS - 0713 447766
HUYU MKINIACHA NAE NUSU SAA HAPA TULIPO NITAMCHAPA NGUMI HAJIELEWI
JUKWAANI
HUYU HATA MKINIACHA NAE HAPA MWAKA MZIMA ATABWABWAJA NA KUNIBWEKEA LAKINI HANG'ATI
WANA-SI - HASA
MUME WANGU TUONGEE KWA AMANI UMENIOA NIKIWA KIGOLI MPAKA SASA NIMEKONGO-LOKA SISIKII KUHUSU DENI LA MAHALI YANGU!
KABLA SIJAJIBU NAOMBA NISEME KUWA. NISIZIKWE HAPA MJINI ALAFU SIMAMIA KABURI LIJENGEWE
YULE DEMU CHAPOMBE WAKO NISHAMFIKISHA KWAKO NARUDI KUMALIZIA BIA YANGU
'UMEUA!' NAVYOMJUA MKE WANGU SIJUI KAMA ZIGO LA MAGENDO BADO LINAPUMUA
JAMANI MIMI NINA DAWA YA KUZINDIKA NDOA, KUZUIA MUME ASIENDE KWA HAWALA NA AKIENDA ASILALE, NA AKILALA ASIMPE HELA, NA AKIMPA HELA SIO ZOTE
ENZI ZANGU MTU HUYU NDUGUZE WANGEMZIKA WAMOTO!
UMEONA KITUONI NDIO SEHEMU SAHIHI YA KWENDA KUNISIFIA GONGO SITII MAJI?
POMBE HAINA ADABU!
SURA SINA HELA SINA MIPANGO SINA MKWARA SINA HATA 'AILAVYU' PIA SINA!
UMETIMULIWA KWA KUMPORO-MOSHEA MINENO MIBOVU DOKTA KISA NINI?
ETI SIRUHUSIWI 'KUNYWA' SABABU NITAHARIBU DOZI WAKATI NINA MWALIKO!
BWANA HARUSI MCHAGA... BI. HARUSI NI MUHAYA...HEBU PATA PICHA
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...UKIPEWA ACHA MASWALI MENGI

# Ulaya haijapata kufundisha ndege vita marubani wa Ukraine

**WASHINGTON,** MAREKANI

MATAIFA ya Ulaya bado hazijapokea kibali rasmi cha Marekani kuanza kuwafunza marubani wa Ukraine kurusha ndege za kivita aina ya F-16.

Kulingana na taarifa zilizochapishwa jana , hawakutajwa majina maofisa wa Marekani na Ulaya waliohusika katika mazungumzo hayo. Hata hivyo, Wizara ya Mambo ya Nje ya Marekani pia bado haijaidhinisha uhamishaji wa nyaraka,vifaa vya ndege vya kompyuta na vifaa vingine.

Takriban nchi 11 za Ulaya zikiongozwa na Uholanzi na Denmark zitashiriki katika mpango wa mafunzo kwa marubani wa vikosi vya wanajeshi vya Ukraine.

Uamuzi wa kuanza kutoa mafunzo kwa marubani wa Ukraine kujadiliwa rasmi wakati wa mkutano wa kilele wa NATO huko Vilnius. Kulingana na chombo kimoja cha habari, maafisa wa Ulaya wanatumaini kuwa programu ya mafunzo itaanza nchini Denmark mapema mwezi wa Agosti, na kituo cha mafunzo pia kitakuwa nchini Romania.

Politico ilisema kuchelewa kuanza kwake kunaweza kusababishwa na sababu za kiufundi, na hakuna ushahidi kwa wakati huu kwamba Marekani haitatoa kibali chake katika siku zijazo.

Hata hivyo, ombi la Ulaya la kuanza mafunzo limekuwa likizingatiwa.

Ofisa wa ununuzi wa silaha nchini Marekani William Laplante, aliiambia Politico katika mahojiano kwamba Idara ya Ulinzi ya Marekani inatoa idhini rasmi ya uhamisho wa nyaraka wakati kila kitu kinapokuwa tayari, ikiwa ni pamoja na tafsiri na mipango ya msaada wa kiufundi.

**BBC**



Mtunza wanyama Vladislav Goncharov, akicheza na simba kwenye bustani ya wanyama jijini Moscow nchini Russia, juzi. **PICHA: EPA-EFE**

# Watoto 289 wafariki dunia wakivuka bahari

**NEWYORK,** MAREKANI

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia watoto UNICEF) limesema kuwa watoto 289, wamefariki dunia katika nusu ya kwanza ya mwaka 2023 wakijaribu kuvuka bahari ya Mediterania kuelekea Ulaya.

UNICEF ilieleza kuwa idadi ya vifo hivyo ni mara mbili zaidi ya rekodi ya miezi sita ya kwanza ya mwaka 2022. Shirika hilo limehimiza kuwekwa kwa njia salama na za kisheria kwa watoto wanaojaribu kuingia Ulaya kwa ajili ya usalama wao.

Afisa wa UNICEF anayehusika na masuala ya uhamiaji Verena Knaus alisema idadi hiyo huenda ikawa kubwa zaidi maana kuna baadhi ya ajali za boti kwenye bahari ya Mediterania ambazo hazinakiliwi.

Knaus aliongeza kuwa katika miezi sita ya kwanza ya mwaka huu, inakadiriwa kuwa watoto 11,600 walivuka bahari ya Mediterania, idadi hiyoni mara mbili katika kipindi kama hicho mwaka uliopita. "Vifo hivi vinaweza kuepukika kabisa," alisema Knaus.

Katika miezi mitatu ya kwanza ya mwaka 2023, watoto wapatao 3,300, sawa na asilimia 71 ya watoto wanaoingia Ulaya kupitia njia ya bahari ya Mediterania, walifanya safari hizo bila ya kusindikizwa na mtu mzima au walitenganishwa njiani.

Idadi hiyo ni mara tatu zaidi katika kipindi kama hicho mwaka jana.

Afisa huyo wa UNICEF alikiri kuwa watoto wengi walikuwa wakifanya safari hizo za hatari wakitumia muda mrefu wakati mwengine au hata miezi ili kufika katika pwani za Libya,

Tunisia na mataifa ya Afrika Kaskazini. Wengi wao walikuwa wakitokea Guinea, Senegal, Gambia, Syria na hata Afghanistan.

Wakiwa njiani, wanaweka maisha yao hatarini na mara nyingi hukabiliwa na visa vya unyanyasaji, ubakaji, biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu huku wasichana wakiwa katika hatari kubwa zaidi.

UNICEF ilisema kuwa safari ya boti kutoka Libya au Tunisia kuelekea Ulaya hugharimu takriban dola za Kimarekani 7,000.

"Hawa watoto wanapaswa kujua kwamba hawako pekee yao, viongozi wa dunia wanafaa kuchukua hatua za haraka kuokoa maisha yao. Salamu za faraja pekee hazitoshi, wanapaswa kuchukua hatua madhubuti na kutafuta suluhu ya kadhia hii," alisisitiza Knaus.

**DW**

# Kiongozi upinzani Senegal aitisha maandamano ya umma

**DAKR,** SENEGAL

KIONGOZI wa chama cha upinzani cha PASTEF, nchini Senegal, Ousmane Sonko, ameitisha maandamano baada ya serikali nchini humo kuzuia mkutano wa hadhara aliopanga kutangaza azma yake ya kuwania urais

Juzi, gavana wa Dakar alitangaza kuwa mkutano huo uliopaswa kufanyika mchana wa jana umepigwa marufuku kutokana na hatari ya kusababisha usumbufu kwa umma.

Kutokana na zuio hilo, Sonko aliwaambia wafuasi wake kuwa, tarehe nyingine kwa ajili ya mkutano huo itatangazwa, lakini akaitisha maandamano yakikusudia kuonyesha hali ya kutoridhishwa na kumtaka Rais Macky Sall aondoke madarakani kwa amani. Sonko alipitishwa kwa kauli moja kwa kura na wanachama wa Chama chake kuwania nafasi hiyo.

Ameteuliwa kugombea nafasi hiyo licha ya kukabiliwa na tuhuma ya kutokidhi vigezo kutokana na rekodi yake ya kukutwa na hatia na vifungo jela.

**DW**

# Uturuki yakumbuka mauaji Julai 15

**ANKARA,** UTURUKI

UTURUKI jana imeadhimisha siku ya demokarasia na umoja wa kitaifa ikiwa ni kwa dhumuni la kuwakumbuka mashujaa wao waliouawa wakati wa jaribio la mapinduzi ya kijeshi lililoandaliwa na kundi linaloitwa la kigaidi la (FETO) kwaajili ya kuipindua serikali iliyokuwa madarakani kipindi hicho.

Aidha, taifa hilo pamoja na balozi zake zote duniani zinaadhimisha kila inapofika Julai 15, kama ishara ya kushidwa kwa jaribio hilo lililokusudia kumuua Rais wa Uturuki na kulipuliwa kwa jengo kuu la Bunge la nchi hiyo. Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Balozi wa Uturuki nchini Tanzania, Dk. Mehmet Güllüoğu, wakati wa maadhimisho ya saba ya jaribio hilo la kuipindua serikali, ubalozi umeandaa programu ya kumbukumbu kwa ajili ya waliofariki siku hiyo, akieleza kuwa walikuwa ni wazalendo waliokuwa wakitetea amani na usalama wa taifa hilo.

"Katika jaribio hilo la kijeshi FETÖ iliuwa raia 251 na kujeruhi 2196 ambao walijaribu kutetea matakwa, amani na usalama wa nchi yao, jumuiya hiyo ni tishio kwa nchi zote ambazo inafanya shughuli zake na tunaendelea kulaani juu ya kile walichokifanya kudhulumu maisha ya watu wasiokuwa na hatia," alisema Güllüoğu.

**DW**

MAKALA

# MALUMBANO NI HATARI KWA UMOJA WETU



Na Magabilo Masambu

**Hakuna jambo jema ndugu mnapoona kuna jambo haliendi sawa mkaitana mezani kwa ajili ya mazungumzo. Sheria nyingi duniani zimetungwa kwa ajili ya wahalifu na hazijawahi kutoa suluhu iliyo njema na mimi siamini kwamba tunashindwa kuitana na kuzungumza.**

SIFA kubwa tuliyokuwa nayo kama nchi ilikuwa juu ya umoja wetu. Majirani na dunia walijua hivyo, ndiyo maana wenye shida na nchi zao sisi tulikuwa washauri na wasaidizi wao. Inawezekana bado tu washauri wao lakini nafikiri sasa wanaweza kuwa wanatutazama tofauti.

Tunajenga nchi kwa manufaa yetu sote na vizazi vyetu. Ya nini tugombanie fito? Pengine wakati mwingine kutotambua wapi fito na miti iliyojenga nyumba yetu ilikotoka linaweza kuwa tatizo. Kuna wakati kutofahamu sawasawa historia ya mafanikio yetu kunaweza kuzaa laana ambayo yaweza kuwa inatufarakanisha bila kujijua.

Kuna umuhimu wa kuwa na mawazo jumuishi. Nikubaliane na kauli ya Rais Samia Suluhu Hassan aliyowahi kuitoa wakati wa mkutano wake na baadhi ya viongozi wa vyama vya siasa hivi karibuni kwamba katika nchi hii hakuna mwenye hatimiliki na kwamba tuishi kwa kuheshimiana.

Ukweli huo unapaswa kuheshimiwa na kila mmoja wetu kwa sababu sheria hazipaswi vilevile kusimamiwa kwa kubaguliwa maana tunaambiwa sheria ni msumeno na kwamba unakata pande zote japo misumeno mingi ninayoifahamu ina makali upande mmoja na upande mwingine ni butu!

Hakuna jambo jema ndugu mnapoona kuna jambo haliendi sawa mkaitana mezani kwa ajili ya mazungumzo.

Sheria nyingi duniani zimetungwa kwa ajili ya wahalifu na hazijawahi kutoa suluhu iliyo njema na mimi siamini kwamba tunashindwa kuitana na kuzungumza.

Mivutano hii inaweza kutumika kama mifupa anayorushiwa mbwa anayemfukuza mwizi mwisho wa siku mwizi hatakamatwa na badala yake mbwa ataendelea kuzubaa akila mifupa hiyo ambayo pia ataishia kuilambalamba tu kwa sababu hana uwezo wa kuitafuna.

Maana yangu ni kwamba leo tuna zaidi ya miaka 60 ya uhuru. Maendeleo tulio nayo leo hatuwezi kujivuna sana japo nakubali kwamba yapo mambo yamefanyika katika ujenzi wa miundombinu, eneo la elimu, afya na maeneo mengine lakini kusema kweli pengine tusingekuwa na hii mivutano na malumbano, tungalikuwa tumepiga hatua zaidi.

Siku tutakayotambua kwamba kila mmoja katika nchi hii ana mchango katika maendeleo ya nchi bila kutazama dini, kabila, chama cha siasa anachotoka na kwamba mawazo na jitihada zake zinatumika na kuheshimika basi, tungalikuwa mbali zaidi ya hapa.

Inawezekana tunayo matatizo katika maeneo ya kisheria, hivyo yatazamwe. Kama ni ya kimaadili, yazungumzwe ili mradi turudi pamoja kama taifa moja lenye nia moja ya kujenga nchi. Bahati mbaya tuliyo nayo ni kwamba nia njema zinazungumzwa lakini hazitekelezwi. Yasiyozungumzwa ndiyo hutekelezwa, yasiyotekelezwa ndiyo yanahitajika, wanaoyahitaji hawayazungumzi.

Pengine hajapatikana refa anayetakiwa kupuliza kipenga wakati timu mbili zinapokuwa uwanjani. Ninachoamini ni kwamba kama kuna watu wawili wamekosana au hawaelewani basi lazima apatikane mtu wa tatu nje ya mahakama za kisheria ili kusikiliza hoja za pande mbili na kuwaunganisha wawili hawa.

Zamani, migogoro mingi katika jamii ilitatuliwa na wazee. Bado naamini wazee hao hawajaisha na bado wapo. Iwe ni migogoro ya kimila au kichama au kiserikali wanaweza kusimama kwenye nafasi zao wakashauri. Ni kwa nini wazee? Kuishi kwingi ni kufahamu mengi. Inawezekana makosa mengine yanatokana na kutoijua historia ya mambo na tukifahamishwa tunasema aaa alah kumbee na mambo yanakuwa yamekwisha.

Kauli na vitendo ni mambo mbalimbali zinaweza kutoka kauli nzuri sana kwa viongozi wetu juu ya umoja wetu, lakini vitendo vikakinzana na ukweli hilo ni tatizo moja tulilo nalo Afrika. Tatizo hili linatokana na utamaduni wa kufundishwa uongo tukiwa wadogo. Mara nyingi tu inatokea kutoa maelekezo kwa watoto kwamba mtu fulani akija mwambieni sipo nimetoka, wakati umelala ndani. Kwa hiyo mtoto tayari anafundishwa kusema asichoamini hata mwenyewe maana anafahamu fika upo.

Naamini kwamba siku tutakapoamua kuzitendea haki hotuba zetu na matamko mbalimbali tukayatekeleza kama tunavyoyasema hadharani, tunaweza kuwa tumetengeneza jambo jema sana ambalo litabaki kwenye historaia ya maisha yetu.

Rais wa Awamu ya Pili, Mzee Ali Hassan Mwinyi, amewahi kusema maisha ni hadithi tu, basi unapoondoka duniani uache hadithi nzuri. Hii ni kwa sababu madaraka yana muda mfupi sana na wameshapita wengi ambao walitisha sana enzi zao lakini zimebaki ama historia nzuri au mbovu kuwahusu wao.

Naamini bado tunayo nafasi ya kuwa wamoja pamoja na tofauti za kimtazamo. Katika hili si lazima tufikiri sawasawa. Kutofautiana ndio uhai wetu lakini usitumike kutugawa. Kila mmoja anatakiwa kujiona kuwa anayo nafasi sawa ya kujiletea maendeleo yake binafsi pamoja na maendeleo ya nchi. Haipaswi kuonekana kwamba wako wanaotakiwa kujenga nchi na wengine wabaki watazamaji. Hilo halitakuwa tofauti na ubaguzi wa aina yoyote ile kama wa rangi na kadhalika.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Wanawake walivyolilia ndoa*



Na Adam Fungamwango

**Wanaume wengi, hapa sasa hata watu wazima wanaingia, wanadai kuwa wanawake wengi siku hizi huonekana kujali zaidi wanaume wenye kipato, hivyo wanaepuka kwa kiasi kikubwa kuitwa 'mwanaume suruali', ndiyo maana kumekuwa na upungufu mkubwa wa wanaume kuoa.**

BAADHI ya wanawake wamekuwa wakilalamika kuwa, wanaume wamekuwa wagumu mno siku hizi kuoa. Wengi hawataki kabisa kuoa na wala kuishi na wanawake ndani kwa staili ya 'sogea tuishi.'

Na ambao watajitahidi sana ndiyo anaweza kumchukua mwanamke na kuishi naye, lakini hapo inawezekana kuoa kabisa ni mpaka nguvu kubwa ya ziada itumike.

Wakati mwingine wapenzi hao wanaachana kabla hata kuoana. Yaani wanaishi pamoja 'kupika na kupakua' hadi wanaachana bila kufunga ndoa.

Wanaume wengi wa sasa ukiwauliza kama ni kweli wanakubali, na ukiuliza sababu wanasema hawataki kujiingiza kwenye ndoa wakati hawana kazi au uhakika na kipato.

Vijana wa sasa wanajisemea ukweli wao kuwa wengi wao kwa sasa hawana ajira na uhakika wa kipato cha kutunza familia, badala yake wanabangaiza, wakipata sawa, wakikosa hewala.

Wanaume wengi, hapa sasa hata watu wazima wanaingia, wanadai kuwa wanawake wengi siku hizi huonekana kujali zaidi wanaume wenye kipato, hivyo wanaepuka kwa kiasi kikubwa kuitwa 'mwanaume suruali', ndiyo maana kumekuwa na upungufu mkubwa wa wanaume kuoa.

Wengine wakasema afadhali zamani ambapo wanaume walikuwa wana kazi ya kusaka pesa ya chakula, akinunua unga, mchele, sukari, maharage, mafuta, dagaa na samaki wakavu akaweka ndani inaweza kumfanya kusaka pesa tu za matumizi madogomadogo sana, tofauti na dunia ya sasa ambayo ina vitu na matumizi mengi kutokana na teknolojia kukua.

Unaweza kununua vitu hivyo vilivyotajwa juu, lakini bado kuna bando la simu mume na mkewe, pamoja na vocha, bili ya maji, umeme, takataka, pesa ya ulinzi, gesi ya kupikia, vifurushi vya ving'amuzi ili familia iangalie tamthilia, watoto katuni na mangine mengi ambayo yote yanahitaji pesa kila uchao.

Kiwango cha elimu cha wanawake ambao kwa sasa wengi wao wameibuka kusaka elimu kwa juhudi kubwa tofauti na zamani na hii imetokana na wazazi wengi kubadili misimamo na mitazamo yao juu ya watoto wa kike ambao zamani alichukuliwa kama kitega uchumi cha kujipatia ng'ombe na mahari hasa vijijini, lakini pia wameonekana ndiyo wanaoweza kuwasaidia zaidi wazazi wao kuliko watoto wa kiume.

Zamani wazazi walikuwa wakikazania kumsomesha mtoto wa kiume kwa madai yeye ndiye atakuwa baba baadaye na kuendeleza familia, lakini baadaye wengi wamekuja kugundua kuwa watoto wao wa kiume wanasaidia zaidi upande wa wake zao, na mabinti zao ndiyo wanaowasaidia hata kwa kidogo wanachokipata.

Hapo wengi wakaamua kuwasomesha wale wanaoonekana kuwasaidia. Mtoto wa kike anapopata pesa husaidia zaidi kwao.

Bado wanawake mpaka leo wanapenda kuolewa, lakini siyo kama vile ilivyokuwa zamani ambapo ilikuwa kama haikuwa hivyo ni aibu yake na ya familia. Leo hii anaweza akaishi peke yake tu na wala jamii haishangai. Mambo yamebadilika.

Haikuwa hivyo zamani. Kuolewa lilikuwa ni jambo la sifa sana na heshima kwa jamii.

Hata tungo nyingi zilielekezea huko.

Tuanze na wimbo 'Kasoro Yangu Sijaijua' ulipigwa na bendi ya MCA International.

"Nitapata lini wangu wa kujivunia, katika masiha nami nijisikie, ninapojaliwa kuolewa mie, sina bahati ya kuishi na mume wangu kwa furaha.

Mpaka leo sijatambua sababu hasa inayofanya wanaume washindwe kuishi na mimi, na mimi sasa mkubwa wajibu kuwa mume, watoto tujipatia watusaidie baadaye.

Vinavyohitajika vyote navitenda ndani, kasoro yangu sijaijua, watoto nawalea nyumba usaji ndugu ninatunza ua, kasoro yangu sijaijua."

Mashairi yameeleweka sipunguzi wala kuongeza kitu.

Wimbo mwingine wa wanawake wanaolalamika kuolewa ni 'Masikitiko' uliotungwa na Kyanga Songa, akiwa na Tuncut Almasi Orchestra.

"Mimi nalia nalie mie oo, najiuliza ni kosa gani nililofanywa kwa Mwenyezi Mola ee.

Uzuri wangu ni wa kuzaliwa nao, pesa ninayo ya kutumia, gari la kutembelea ninalo, nyumba nzuri ya kulala ninayo ooo mama.

Kinachonisikitisha ni kuona kwamba nakosa mume wa kunioa, mama, nami nijisikie kama wenzangu waliobatika kuolewa.

Hata wa kunisabahi njiani simpati, hata wa kunipa jambo ya bure njiani simpati, mikosi gani nalizaliwa nayo mie wao, masikini mama iyolele?" Anauliza mtoto wa kike.

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

# Kafie kwenu-2

CAROLINA, binti mrembo, aliyeumbwa akaumbika, mwenyewe anajiita Carry. Akifahamu fika jinsi alivyo mzuri na kubabaisha kila mwanaume anayekutana naye barabarani, anageuka kuwa mtu mwenye kiburi, jeuri, dharau na majivuno kwa watu. Atamsalimia yule tu aliyempenda kumsalimia. Ataongea na mtu atakayemchagua na si kila mtu. Anaweza kuziba hata pua akipita mtu ambaye yeye anaona si wa hadhi yake. Si mwanaume wala mwanamke. Jirani na anapoishi, kuna kijana mgeni asiyepungua miaka 25 hivi aliyehamia hivi karibu eneo la Kinondoni Moscow. Anaitwa James. Alikuwa kijana anayeishi maisha ya hali ya chini, akipanga chumba kimoja. Jicho lake naye liliona urembo wa Carry. Akaamua kujaribu. Kilichompata hatosahau maishani mwake. Fuatilia hadithi hii ya kusikitisha, kuhuzunisha, kufurahisha, kuburudisha na kufundisha kwa wakati mmoja.

**Na Adam Fungamwango (0716 350534)**

AKIWA anatoka kununua mihogo ya kukaanga kwa mama binti Mshindo, alikatisha kichochoro kimoja na kukutana na wasichana wawili. Alisimama na kuwatazama. Ni kama walifanana hivi. Lakini macho yake yakaganda zaidi kwa mmoja bila sababu yoyote ile.

Walikuwa wanatembea kwa madaha mithili ya twiga mbugani. Kwa muda aliyowatazama alijikuta akipata burudani ya akili ya mwili. Ni kama presha yake ilikuwa imeshuka hivi. Mwili wake ulisisimka kama mtu ambaye anayesikiliza muziki mzuri anaoupenda.

"Hawa ni binadamu, au malaika," alijiambia mwenyewe. Mpaka wakati huo alikuwa amesimama.

Hakuwa na nguvu za kutembea.

Alikuwa amesimama pembeni kama mtu ambaye alikuwa anawapisha wapite.

Ndiyo muda ambao alipata wasaa wa kuwatazama vizuri warembo hao. Kila walipokuwa wakikaribia harufu ya manukato ilizidi kumchanganya.

Akiwa na bakuli lake lililojaa mihogo alibaki ameduwaa mpaka wasichana hao walipomfikia.

"Habari zenu warembo."

Hakusikia sauti yoyote iliyomjibu. Mmoja alimtazama kuanzia chini, akampandisha hadi juu. Macho pekee yalikuwa na sauti tosha. Waliongea. Hakupenda kabisa salamu hiyo. Alipomaliza kumtazama kwa dharau, akaishia na kufyonya.

Mmoja aliyebaki hakujibu chochote na wala hakuitikia salamu. Alibaki anamtazama mwenzake.

James hakujali, kukasirika wala kupata presha na kilichotokea. Wala hakujibu fyonyo hilo kwa maneno makali au hasira.

Alibaki kimya na kutabasamu. Kwa maisha anayoishi James, hilo kwake ni jambo alilolizoea kabisa.

Ameshawahi kudhalilishwa mara 10 zaidi ya alivyofanya yule msichana.

Ameshawahi kumwagiwa mpaka maji ya ukoko na mambo mengine mengi ambayo yamebaki kuwa siri yake moyoni.

Kwa ufukara na mwonekano wake hilo ni jambo la kawaida sana. Ni kama msichana yule hakufanya kitu chochote ambacho kingemkasirisha James. Kama msichana yule alifanya vile ili kumkasirisha alikuwa amenoa.

*************************************

Taarifa zilivuja. Kama kawaida waliovujisha waliongeza na chumvi juu.

Vijana wa kiume, wa kike na kinamama karibuni eneo zima la Kinondoni Moscow lilipata umbea kuwa James alimtongoza Carry.

Ikawa ni simulizi ya kushangaza na kuchekesha kwa wakati mmoja. "Kweli jamani kweli? Yaani James kamtongoza Carry?" Walijiuliza.

Hakuna hata mmoja aliyejiuliza matokeo yalikuwaje. Kila mtu anajua kilichotokea hata kama hajaona. Carry hakuwa mwanamke wa kawaida. Hagusiki.

Ni msichana mkali, jeuri, kejeli na dharau asiyemuogopa yeyote yule na mwenye kujiamini.

Kama hakuna mwanaume yeyote pale aliyempata sembuse James! Historia yake alipotoka haijulikani sana, lakini alihamia hapo miaka miwili na nusu iliyopita.

Yeye na mdogo wake Catherine ambaye anajulikana zaidi kwa jina la Catty wamepanga kwenye moja kati ya nyumba za kisasa Kinondoni Moscow.

Nyumba yao ilikuwa na geti kubwa jeusi kiasi kwamba walionekana wakitoka, kuingia na kutembea njiani, tena si kwa umbali mrefu kwani walikuwa wanachukua bodaboda au bajaj.

Carry alikuwa mkubwa miaka miwili zaidi ya mdogo wake Catty. Majirani wanasema mwenye matatizo ni Carry, lakini mdogo wake hana tabia mbaye kama dada yake. Yeye anaonekana yupo tofauti, lakini kinachomfanya aonekana ana tabia zinazoendana na dada ni kwamba yeye ni mdogo na mambo mengi ni lazima amsikikilze mkubwa wake.

Hana tabia ya kujibu watu vibaya wala kuwaangalia kwa dharau, na inaonekana hapendi tabia za dada yake, lakini yeye ni mdogo atafanyaje?

Wanasema mara chache chache akiwa peke yake anapopita huwa anasalimia watu na kujibu salamu za watu, lakini anapokuwa na dada yake ndipo anapokuwa kimya akimhofia mkubwa.

Majirani wanabainisha kuwa Carry na Catty wanafanya kazi kwenye hoteli moja kubwa katikati ya Jiji la Dar es Salaam kama wahudumu.

Kazi yao na uzuri waliojaaliwa nao, ukichanganya na urembo wanaojiweka na mavazi ya gharama wanayovaa yanawafanya kuwa kivutio kwa wanaume wengi.

Tatizo ni kwamba hata wanaume ambao wanaona si hadhi yao nao wanajichomeka humo humo.

Jioni moja tulivu, kama kawaida ya wanawake wengi wa uswahilini wanakuwa wamekaa vibarazani baada ya chakula cha mchana.

Baadhi yao hawana kazi yoyote ya maana zaidi ya kusema na kusengenya watu.

Wao watamchambua yoyote atakayepita na hasa wanayemfahamu.

Wao hawana kizuri. Akipita mrefu atachambuliwa ubaya wa urefu wake na mfupi ndiyo kabisa atanangwa huku mwenyewe akipita bila kujijua.

Akiwa mweupe utatafutwa ubaya wa kuwa mweupe popote pale ili mradi tu wapate cha kuongea na akiwa mweusi basi hata hawapati tabu kumsasambua.

"Weusi kama mafuta ya breki, kama mkaa, au ukuta wa jiko, au mweusi kama usiku wa balaa."

Mtu akiwa mwembamba ataambiwa ana virusi vya ukimwi, na akiwa mnene bado, ataambiwa anatumia dozi ndiyo maana amenenepa.

Haya ndiyo maisha ya baadhi ya kinamama wa uswahilini hasa wasiopenda kujishughulisha na kazi yoyote, kazi kukaa na kusema ya wenzao, wakati nao wana matatizo mengi tu yaliyowashinda, lakini wala hawayaoni.

Kazi yao akipita mtu anaanza kuchambuliwa ukucha hadi unywele bila yeye kujijua.

Wakati wakimnanga dada mmoja aliyepita dakika moja iliyopita kuwa gauni lake zuri, lakini rangi yake maji ya kunde haikuendana na nguo hiyo, pia ingekuwa ndefu kidogo lakini kaifanya fupi wakati miguu yake myembamba kama ufagio wa site, na hata viatu alivyovaa ni fasheni ya kizamani, vimeshapitwa na wakati.

Wakati huo ndiyo James naye alikuwa anapita kutoka kwenye mihangaiko yake akiwa na uchovu kutokana na kazi ngumu alizotoka kuzifanya.

Kinamama na kinadada wakamuacha yule dada, wakaanza kumuongelea kijana wa watu juu ya kilichojiri mtaani hapo siku mbili zilizopita kuwa alimtongoza Carry, lakini vipande alivyopewa hatorudia tena.

**ITAENDELEA JUMAPILI**




**Yeye na mdogo wake Catherine ambaye anajulikana zaidi kwa jina la Catty wamepanga kwenye moja kati ya nyumba za kisasa Kinondoni Moscow. Nyumba yao ilikuwa na geti kubwa jeusi kiasi kwamba walionekana wakitoka, kuingia na kutembea njiani, tena si kwa umbali mrefu kwani walikuwa wanachukua bodaboda au bajaj.**



# WOSIA MZITO

WANAISHI kama marafiki, lakini ukweli ni mama na bintiye, ndivyo Mwigizaji wa Bongo Muvi Kajala masanja na Binti yake Paula wanavyoishi kila siku.

Ukiangalia katika kurasa zao za mitandao ya kijamii utakumbana na picha za Kajana na Paula, wakiwa katika maisha ya furaha kama marafiki zaidi na kuachana na ukaribu wa mama na mtoto.

Kiujumla masha ya mastaa hao ni ya siafu kila wakati huwa pamoja, hakuna mtu anayeweza kuwatenganisha kwani linalomfurahisha ndilo linalompa raha Paula.

Hivi karibuni paula ameshereheka miaka 21 ya kuzaliwa kwake, Kajala kama kawaida hakutaka kuwa mbali na mtoto wake, kwani amejikuta akiyatoa maneno mazito.

Akizungumza na millardayo, amesema kitu pekee ambacho Paula anatakiwa kuelewa ni kwamba maisha sawa na dhoruba kali, kama hatakuwa imara kukabiliana nayo basi ataanguka.

'Kwako dada Pau, mtoto wangu wa pekee maisha yatakuwa na misukosuko, majaribu na tabu tele. Ila hakikisha tabasamu lako na furaha yako inakuwepo na wewe popote uendapo,"amesema kajala.

Akaongeza "Nataka tu ufahamu wewe ni kitu changu cha thamani cha pekee nilichowahi kuwa nacho hapa duniani. Daima nilikuwepo, nipo na nitaendelea kuwepo kwenye maisha yako kukulinda na kukupigania kwa kila baya.

# Uibuaji vipaji Tabora waanza

MSANII anayechupukia katika Bongo Fleva kutoka mkoa wa Tabora, Nzige Boy ameweka wazi mpango wake wa kutaka kuwasaidia vijana wenzake kwa kuibua vipaji vipya.

Akizungumza na BT, meneja na prodyuza wa Nzige Boy, Manjay Killer, amesema mpango huo tayari umeanza kuwavutia wadau wa sanaa kutoka sehemu mbalimbali.

"Sisi tumejipanga kuhakikisha wasanii wetu wanakuwa tofauti na wasanii wengine, tunashirikiana na Full Tank Comedian, Alex Machejo na Mudy Sound kuhakikisha tunafanya mapinduzi katika mkoa wetu wa Tabora," amesema Manjay Killer.



# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

**PSG YAMKOMALIA KANE**
KLABU ya Paris St-Germain inajaribu kuteka nia ya Bayern Munich kwa mshambuliaji wa Tottenham Hotspur na Timu ya Taifa ya England, Harry Kane, mwenye umri wa miaka 29. (***Independent***)

**PAVARD ANUKIA CITY**
KLABU ya Manchester City imemfanya beki wa pembeni wa Bayern Munich na Ufaransa, Benjamin Pavard, mwenye umri wa miaka 27 kuwa shabaha yao kubwa kama mlinzi wao huku Kyle Walker (33), atajiunga na mabingwa hao wa Ujerumani. (***Guardian***)

**AUBAMEYANG KUTUA MARSEILLE**
KLABU ya Marseille inajaribu kumsajili mshambuliaji wa Gabon, Pierre-Emerick Aubameyang, mwenye umri wa miaka 34 kutoka Chelsea. (***Relevo***)

**CAICEDO ATAJWA LIVERPOOL**
LIVERPOOL itafikiria kujiunga na kinyang'anyiro cha kumsajili kiungo wa kati wa Brighton na Ecuador, Moises Caicedo, mwenye umri wa miaka 21 kama Jordan Henderson na Fabinho watahamia Saudi Arabia. (***Talksport***)

**HENDERSON NJIA MOJA**
LIVERPOOL inatarajiwa kukubali ada ya takribani pauni milioni 10 kwa ajili ya kumuuza kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya England, Henderson, mwenye umri wa miaka 33 kwa Al Ettifaq. (***Football Insider***)

**FULHAM YAMBANI MITROVIC**
FULHAM imekataa ofa ya pili kutoka kwa Al Hilal kwa ajili ya kumnunua mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Serbia, Aleksandar Mitrovic, mwenye umri wa miaka 28. (***90min***)

**FULHAM, WEST VITANI**
KLABU za Fulham na West Ham zipo katika mbio ya kuwania huduma ya James Ward-Prowse, msimu huu wa joto, ingawa Southampton bado hawajapokea ofa kwa kiungo huyo wa kati wa England mwenye umri wa miaka 28. (***Football Insider***)

**OSIMHEN KUMBAKISHA MBAPPE**
PSG inamlenga mshambuliaji wa Napoli na Nigeria, Victor Osimhen mwenye umri wa miaka 24, sio kuchukua nafasi ya Kylian Mbappe, lakini kusaidia kumshawishi mshambuliaji huyo wa Ufaransa kubakia klabuni hapo. (***Sport***)

**VILLA KUMUUZA DIGNE**
ASTON Villa itasikiliza ofa kwa, Lucas Digne, huku Napoli ikiwania kumsajili mlinzi huyo wa kushoto wa Timu ya Taifa ya Ufaransa mwenye umri wa miaka 29. (***Mundo Deportivo***)

**DIABY KUIKAMUA LEVERKUSEN**
BAYER Leverkusen imeiambia Aston Villa italazimika kuvunja rekodi yao ya uhamisho ili kumsajili winga wa Ufaransa, Moussa Diaby, mwenye umri wa miaka 24. (***Talksport***)

**DIALO KUTUA BRENTFORD**
KLABU ya Brentford imewasilisha dau la pauni milioni 13 kwa ajili ya kumnunua mchezaji wa Strasbourg, Habib Diallo, huku wakitarajia kushindana na West Ham kwa mkataba wa mshambuliaji huyo wa Senegal mweye umri wa miaka 28. (***Football Insider***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# ARSENAL YANAFIKIWA KUMSAJILI TIMBER

**LONDN,** Arsenal

### Arteta anaamini beki huyo chipukizi ameshaiva na ataisaidia timu...

ARSENAL imekamilisha usajili wa beki, Jurrien Timber, kutoka Ajax, klabu hiyo imetangaza.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, ambaye anaweza kucheza beki wa kulia au beki wa kati, amesaini mkataba wa muda mrefu na klabu hiyo ya London Kaskazini.

**Ajax ilithibitisha klabu zote mbili zilikubali ada ya uhamisho ya euro milioni 40 ambayo inaweza kuongezeka hadi kufikia euro milioni 45 kupitia vigezo.**

"Tunafurahi sana Jurrien amejiunga nasi," alisema Kocha wa Arsenal, Mikel Arteta, alisema katika taarifa yake.

"Ni beki chipukizi anayeweza kubadilika, ambaye atafaa katika mfumo wetu na kukipa kikosi chetu ubora wa ziada.

"Jurrien ni mchezaji mwenye umri mdogo, lakini tayari amepata mafanikio makubwa. Amepata uzoefu wa kushiriki michuano mikubwa ya kimataifa kwa zaidi ya mara moja, pamoja na mataji aliyoshinda akiwa na Ajax. Tunatarajia kuwakaribisha na kumuunganisha Jurrien kwenye kikosi."

Arteta amekuwa na nia ya kuimarisha safu yake ya ulinzi baada ya timu yake kutokuwa na wakati mzuri kutokana na kukosekana kwa Wlliam Saliba mwishoni mwa msimu uliopita, na hatimaye kupoteza mbele ya Manchester City katika mbio za kuwania taji la Ligi Kuu England msimu uliomalizika.

Kai Havertz tayari amejiunga na Arsenal msimu huu akitokea Chelsea kwa mkataba ambao ESPN iliripoti kuwa una thamani ya hadi pauni milioni 67.5.

Vyanzo vimeiambia ESPN kwamba Arsenal wamekubali mkataba na West Ham United kwa Declan Rice baada ya City kujiondoa kwenye mbio za kumsajili kiungo huyo.

Akizungumza na tovuti ya klabu hiyo, Timber alisema: "Ilikuwa ni kwa sababu ya kaka zangu. Siku zote walikuwa mashabiki wa Arsenal, na nilipenda tu kuona Arsenal wakicheza. Walikuwa na wachezaji wakubwa, jinsi walivyocheza, mtindo. Naipenda klabu tu.

"Nilikuwa na hili tangu nikiwa mdogo, lakini kaka zangu waliniwekea hilo. Nilipenda kuwatazama Robin van Persie bila shaka, na Thierry Henry. Walikuwa wachezaji wangu ninaowapenda."

## Mendy sasa afutiwa mashtaka ya ubakaji

**LONDON,** England

MCHEZAJI wa zamani wa Manchester City, Benjamin Mendy (28), amefutiwa mashtaka ya kubaka.

Mendy alishtakiwa kwa kumshambulia mwanamke mwenye umri wa miaka 24 katika jumba lake la kifahari huko Mottram St. Andrew, Cheshire mnamo Oktoba, mwaka 2020.

Nyota huyo pia alishtakiwa kwa jaribio la kumbaka mwanamke mwingine, mwenye umri wa miaka 29, ambaye pia alisema alimdhalilisha nyumbani kwake miaka miwili kabla.

Hiyo imekuja baada ya kuondolewa makosa sita ya ubakaji katika kesi ya awali Januari.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa aliangua kilio wakati hukumu ya kutokuwa na hatia ikisomwa na msimamizi wa mahakama kufuatia kesi iliyodumu kwa wiki tatu katika Mahakama ya Chester Crown.

Jopo la Mahakama la majaji 12 lilijadili kwa takriban saa tatu na dakika 15 kabla ya kufikia hitimisho hilo.

Jaji, Steven Everett, alisema: "Mendy anaweza kuachiliwa kutoka kizimbani."

Mwanasoka huyo, ambaye mkataba wake na Manchester City ulimalizika mapema mwezi huu, aliondolewa katika kesi ya awali ya makosa sita ya ubakaji na shitaka moja la unyanyasaji wa kingono, unaohusisha na wasichana wanne.





# AL-AHLI YATUMA OFA KWA MAHREZ

**RIYADH,** Saudi Arabia

KLABU ya Saudi Arabia Al-Ahli iko tayari kupeleka ofa ya pauni milioni 30 ili kumsajili, Riyad Mahrez, kutoka Manchester City, kwa mujibu wa ESPN.

Waarabu hao wako tayari imetoa ofa ya pauni milioni 25 kwa mwaka kwa Mahrez, kwa mujibu wa gazeti la The Athletic, na lazima sasa washawishi mabingwa hao wa Ulaya kumuuza mchezaji huyo.

City wanadaiwa wanataka kumbakiza mchezaji huyo ambaye amebakiza miaka miwili kwenye mkataba na klabu hiyo ya Etihad.

Ingawa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 alikosa nafasi mbele ya Bernardo Silva msimu uliopita, Mreno huyo anatazamwa kama mbadala wa Ilkay Gundogan aliyeondoka kuelekea Barcelona.

Hiyo ina maana Mahrez bado anakuwa na jukumu muhimu la kucheza huku kikosi cha Pep Guardiola kikilenga kutetea mataji matatu msimu ujao.

Tangu asajiliwe kutoka Leicester mwaka 2018, winga huyo ameshinda mataji manne ya Ligi Kuu England, mawili ya FA, matatu ya Kombe la EFL na Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Amefunga mabao 78 katika mechi 236 katika miaka yake mitano katika klabu hiyo.

# *Ancelotti kubadili mfumo Madrid*

**MADRID,** Hispania

CARLO Ancelotti amesema ana mpango wa kujaribu kikosi kipya wakati wa ziara ya Real Madrid nchini Marekani mwezi huu, huku kocha huyo akitafuta kuwajumuisha wachezaji wapya kama Jude Bellingham kwenye timu kabla ya msimu wa 2023-24.

Katika msimu wa joto wenye shughuli nyingi hadi sasa kiungo Bellingham, Joselu, Arda Guler na Brahim Díaz na beki wa pembeni, Fran García wamejiunga na Madrid, huku Karim Benzema, Marco Asensio, Eden Hazard na Mariano Díaz wakiondoka baada ya mikataba yao kumalizika.

"Nilipoanza kufundisha nilikuwa na wazo, na sikuzoea wachezaji niliokuwa nao," alisema Ancelotti akiwaambia waandishi wa habari, alipoulizwa kama atazingatia mabadiliko ya mfumo.



"Nilikuwa na uzoefu kule Parma, ambapo (Roberto) Baggio alitaka kucheza kama kiungo mchezeshaji na sikubadilisha mfumo. Alienda timu nyingine. Na nilikosea."

Biashara ya Madrid majira ya joto inamaanisha kikosi kwa sasa kimejaa zaidi katika safu ya kiungo, na wachezaji wasiopungua saba,wote wakiwania nafasi.

Ancelotti amekuwa akipendelea mfumo wa 4-3-3 muda wote akiwa Madrid, lakini kumekuwa na uvumi kwamba usajili wa Bellingham unaweza kuashiria kubadilika kwa mfumo.

"Mwaka huu tunaweza kucheza mfumo tofauti. Mfumo ambao tumecheza nao umekuwa na mafanikio makubwa, lakini tunaweza kujaribu mtindo mpya. Tutaujaribu kwenye ziara. Ni wakati mzuri kufanya hivyo."

HABARI MICHEZO

# AZAM YAANZA KUONYESHA MAKALI YAKE KWA AL HILAL

**Na Adam Fungamwangobo**

USHINDI wa mabao 3-0 ilioupata Azam FC katika mechi ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya Al Hilal ya Sudan iliyochezwa kwenye Uwanja wa Rades, nchini Tunisia juzi, ni dalili za kuimarika kuelekea msimu mpya na mechi za kuwania Ngao ya Jamii.

Wachezaji wapya wawili raia wa Senegal, Cheikh Sidibe na Alassane Diao walifungua akaunti zao za magoli wakati bao lingine lilipachikwa na Prince Dube.

Kiungo mshambuliaji mpya wa timu hiyo, Feisal Salum 'Fei Toto' aliyesajiliwa akitokea Yanga naye ameanza kwa makeke kwa kutoa 'assist' ya bao la kwanza lililofungwa dakika ya tisa na Sidibe.

**Mzimbabwe Dube aliongeza bao kipindi cha pili dakika ya 53, kabla ya straika mrefu, Diao, aliyesajiliwa pia msimu huu akitokea US Goree ya Senegal.**

Timu zote hizo mbili zipo Tunisia kwa ajili ya maandalizi ya msimu mpya ambao hapa nchini utaanza Agosti 15, mwaka huu.

Ofisa Habari Msaidizi wa Azam FC, Hasheem Ibwe, amesema matokeo hayo waliyopata na kipimo cha mechi ni sababu mojawapo iliyowafanya kuweka kambi nje ya Tanzania ambapo wanaamini wachezaji hupata utulivu mkubwa.

"Lile swali kwa nini Azam wanakwenda kuweka kambi nje ya nchi sasa limeanza kujibiwa, maana yetu ilikuwa ni hiyo, kucheza na timu ambazo zina uzoefu katika michuano ya kimataifa na hata msimu ujao zitashiriki pia, kwa sababu na sisi tunacheza mechi za kimataifa tunataka kujipime tuone kiwango chetu kiko wapi, tumefika wapi na tunatakiwa tuboreshe vipi na wapi," alisema Ibwe.

Ofisa huyo aliongeza baada ya mechi hiyo ya juzi, Azam FC pia inatarajia kupata michezo mingine ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya CS Sfaxien, US Monastir na Esperance, zote za Tunisia, endapo watakubali maombi yao.




Mjumbe wa Kamati ya Utendaji ya Yanga, Yanga Makaga (katikati), akionyesha kadi ya uanachama ya klabu hiyo baada ya kukabidhiwa katika uzinduzi wa Wiki ya Mwananchi uliofanyika kwenye Uwanja wa Furahisha jijini, Mwanza jana. **PICHA: MTANDAO**

## Yanga kushusha mashine mpya

INATOKA UK. 24

moto na kupandisha ubora wa wachezaji waliopo, huku akisisitiza Yanga ndio timu pekee Tanzania iliyokuwa na kikosi bora ambacho kilifanya makubwa msimu uliopita.

"Sisi tunasajili wachezaji ambao wataleta changamoto tu kutoka pale ambapo tulikuwa msimu uliopita, kupandisha ubora wetu kuelekea msimu unaofuata, kama tulifanya vizuri kwenye michuano mbalimbali iliyopita lazima tutengeneze nafasi za ushindani kwenye kikosi, hakuna ambaye atabweteka, na huu ushindani wa namba ndio utasababisha tufanye vizuri zaidi katika michuano ya ndani ya kimataifa," alieleza kiongozi huyo.

Hata hivyo alisema wanatarajia kuwaacha baadhi ya wachezaji na wengine kuwatoa kwa mkopo katika timu mbalimbali ambazo watafikia makubaliano.

"Hakuna mchezaji tunayemfukuzia hivi sasa, tayari tumeshamaliza usajili kilichobaki ni kuwatangaza tu, na wale ambao tutawatoa kwa mkopo au kuwaacha tutawapa taarifa zao hivi karibuni," alibainisha.

Taarifa zilizopatikana zinasema beki wa kulia, Djuma Shaaban, raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), huenda akakumbana na mkono wa kwaheri baada ya nafasi yake kupatikana nyota mpya.

Yao anakuwa mchezaji wa pili kusajiliwa na Yanga kutokea Asec Mimosas baada ya msimu uliopita kumnasa, Stephane Aziz Ki wakati watani zao Simba wamemsajili, Aubin Kramo Kouame (27) kutoka klabu hiyo hiyo.

## *Kuogelea waipigia magoti serikali*

**Na Shufaa Lyimo**

CHAMA cha Kuogelea Tanzania (TSA), kimeiomba serikali kuwekeza zaidi katika mchezo huo ili wachezaji wake wafanye vizuri katika mashindano mbalimbali ya ndani na nje ya nchi wanayoshiriki.

Hayo yalisemwa jana na Kocha Mkuu wa Timu ya Taifa ya Kuogelea, Alexander Mwaipasi, katika semina ya waandishi wa habari za michezo iliyoandaliwa kwa lengo la kuwaongezea ufahamu na kuzijua sheria za mchezo huo.

Mwaipasi alisema anawataka Watanzania wajitokeze kushiriki katika mchezo huo na kuondoa dhana kuwa ni maalumu kwa watu wenye uwezo mkubwa wa fedha.

"Tumeamua kuwapa mafunzo haya baada ya kuona waandishi wengi wanaripoti mchezo huu huku hawafahamu sheria zake," alisema Mwaipasi.

Naye Rais wa TSA, Noel Kiunsi, aliliambia gazeti hili wanaiomba serikali na wadau kusaidia kupata vifaa na kuboresha miundombinu ili wafundishe aina mbalimbali za kuogelea kama wanavyofanya nchi nyingine.

"Mchezo huu ulianza kabla ya Uhuru na tukafanikiwa kukisajili chama cheti ilipofika mwaka 2007, hivyo tunatamani Watanzania wengi waujue mchezo wetu," alisema Kiunsi. Aliongeza kutokana na changamoto ya miundo mbinu, Tanzania unachezwa mchezo mmoja kati ya aina saba zilizopo.

"Tunaiomba serikali itusaidia katika kuboresha vifaa, Tanzania inapata nafasi mbalimbali za kushiriki mashindano ya kimataifa tofauti na mchezo wa mpira wa miguu, na hii inatokana na juhudi zinazofanywa na uongozi wetu," Kiunsi aliongeza.

## Simba SC kutambulisha

INATOKA UK. 24

timu yao nafasi ya kujiandaa na nusu fainali ya Ngao ya Jamii utakayochezwa jijini, Tanga.

"Safari hii jezi zetu mpya tunaenda kuzizindua kihistoria juu ya kilele cha Mlima Kilimanjaro, itakuwa siku ya Ijumaa na baada ya uzinduzi tu zitaanza kuuzwa rasmi katika maduka yote," alisema Kajula.

Naye Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema atakuwa sehemu ya wataoongoza msafara wa uzinduzi wa jezi katika kupanda mlima.

Alisema tiketi na mipango yote kuhusu tamasha hilo na utaratibu wataviweka hadharani wakati wowote kuanzia sasa na kuongeza utaratibu utafanyika kisasa.

"Usajili unaendelea, bado mchezaji mmoja na viongozi wa Simba wasikivu sana, sasa ni zamu ya mmakonde (Luis Miquissone) usajili ambao wanaousubiri Wanasimba kuuona kwa sasa.

Kwa sasa Simba kuna mmakonde mmoja (mimi), bado mmakonde mwingine kutua ndani ya kikosi cha Simba, vuta picha kikosi yupo Aubin (Kramo), Willy Essomba Onana, Jean Baleke halafu kuna Miquissone," alisema na kuongeza;

Safari hii wapinzani wajiandae maana Simba ni tishio ukiachilia nyota hao, kuna Clatous Chama, ambaye kuna watu wanamuota na wataendelea kumtamani tu hawampati".

Naye mshambuliaji mpya wa Simba, Onana alisema anaushukuru sana uongozi wa klabu hiyo na amewahakikishia mashabiki watapata furaha na burudani kwa sababu wamejipanga kupambana ili kufikia malengo yao.

"Siwezi kuzungumza sana kwa sababu kazi yangu itaonekana uwanjani, nitajitahidi kadri ya uwezo wangu kufanya kila kitu pamoja na wachezaji wenzangu ili kuwapa furaha mashabiki," alisema Onana.

Kaimu Mtendaji Mkuu wa NMB, Filbert Mponzi, alisema ushirikiano kati ya Simba na benki yao utakuwa na mafanikio makubwa kwa mashabiki wa klabu hiyo.

Mponzi alisema katika ushirikiano huo utawanufaisha mashabiki na wanachama kufungua Akaunti ya Simba, Queens (Malkia kwa Wanawake), Platinum na Watoto.

"Kadi moja itatumika katika utambulisho wa wanachama wa klabu ya Simba na kufanyia muamala, pia watafaidika kwa kupata bima ya maisha au ulemavu na kupata mkopo haraka, tutakuwa na akaunti ya watoto," Mponzi aliongeza.

# Michezo

Jumapili Julai 16, 2023

Nipashe




Al-Ahli yatuma ofa kwa Mahrez UK. 22




Mwenyekiti wa Simba, Murtaza Mangungu (wa pili kushoto), akiwa na viongozi wengine wa klabu hiyo pamoja na wawakilishi wa Benki ya NMB baada ya kuzindua ushirikiano na benki hiyo katika halfa maalumu iliyofanyika Dar es Salaam jana. **PICHA: SAADA AKIDA**

# YANGA KUSHUSHA MASHINE MPYA

## ●●● Ni winga Skudu kutoka Marumo Gallants huku Mkongomani Djuma akipewa...

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

BAADA ya kufanikisha usajili wa beki kutoka Asec Mimosas ya Ivory Coast, Kouassi Attohoula Yao, mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara wako katika mazungumzo na winga wa Marumo Gallants FC ya Afrika Kusini, Mahletse Makudubela 'Skudu', imeelezwa.

Taarifa kutoka Yanga zinasema wao wamepewa mkataba wa miaka miwili na rasmi sasa atakuwa katika kikosi cha Jangwani kuelekea msimu mpya wa mwaka 2023/2024.

Chanzo kutoka Yanga kinasema viongozi wa klabu hiyo pamoja na wawakilishi wa winga huyo wako katika hatua za mwisho za mazungumzo na wanaamini usajili huo utaendelea kuimarisha kikosi chao ambacho hakitakuwa na mabadiliko makubwa.

"Ni kweli winga huyo yuko katika mazungumzo na Yanga, na mambo yakienda sawa sawa atakuwa sehemu ya kikosi cha timu yetu," kilisema chanzo chetu.

Tayari Yanga imeshakamilisha usajili wa wachezaji watano wapya ambao wengine ni Nickson Kibabage , Gift Freddy, Max Pia Nzengeli na Jonas Mkude, nyota wote hao wameshaingia kambini kwa ajili ya kuanza maandalizi ya msimu ujao.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, alisema wamekamilisha usajili wao na uamuzi huo umetokana na mapendekezo yaliyotolewa na Kocha wao mkuu, Miguel Angel Gamondi.

Kamwe alisema, bado hawajamaliza mchakato huo na watakamilisha usajili wa wenye lengo la kuimarisha kikosi chao pale watakaponasa saini ya 'kifaa hatari' kipya.

"Yao ni jeshi kubwa, tumeimarisha na kuongeza nguvu safu yetu ya ulinzi, tumesajili beki hatari na ameingia kambini kujiunga na wachezaji wenzake katika maandalizi ya msimu mpya wa mashindano," alisema Kamwe.

Aliongeza kabla ya kucheza mechi hiyo ya Ngao ya Jamii, Gamondi atapata mechi kadhaa za kirafiki ikiwamo mchezo wao wa kirafiki wa kimataifa dhidi ya Kaizer Chief ya Afrika Kusini utakaofanyika katika Siku ya Mwananchi ifikapo Julai 22, mwaka huu.

"Mechi hizo zitampa nafasi kocha wetu kuona madhaifu ya kikosi chake na kufanyia kazi haraka kabla ya ligi kuanza, mechi ya Kaizer Chief itakuwa ya wazi yenye lengo la kuwapa mashabiki wao nafasi ya kuona ubora wa wachezaji wapya tuliowasajili msimu huu," Kamwe alisema.

Aliongeza usajili wanaofanya sasa utaongeza changamo-

INAENDELEA UK. 23

## Simba SC kutambulisha jezi Mlima Kilimanjaro

**Na Saada Akida**

WAKATI uongozi wa Simba umesema utatambulisha rasmi jezi yake mpya itakayotumika katika msimu mpya wa 2023/2024 katika kilele cha Mlima Kilimanjaro, Tamasha la Simba mwaka huu litafanyika Agosti 6, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Uzinduzi wa jezi hiyo utafanyika saa 1:00 usiku Julai 21, mwaka huu na mchakato wa mauzo utaanza muda mchache baada ya uzinduzi huo.

Akizungumza na Nipashe jana katika hafla ya ushirikiano pamoja na Benki ya NMB, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Imani Kajula, alisema sababu ya kuzindua jezi kwenye mlima Kilimanjaro ni kutokana na umaarufu wa mlima huo na ukubwa wa klabu hiyo ambayo ipo katika nafasi ya saba kwa ubora wa Afrika.

Kajula alisema pia wameamua kurudisha nyuma Tamasha ya Simba Day kwa lengo la kuipa

INAENDELEA UK. 23

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042